

MAJI YALIYOPO DAIMA

YATOKAYO MWAMBANI



Tunashukuru asubuhi ya leo kwa ajili ya Uwepo wa Bwana Mungu, ambao ungeanzisha ibada za mapema kwa kutupa ujumbe, kwamba—kwamba inatupasa “kusikiliza, kuwa na kicho” mbele Zake, kwamba ana jambo la kutuambia. Nina hakika kwamba atafanya lile ambalo ameahidi. Yeye daima hulitimiza Neno Lake. Na kwa hiyo tunashukuru kukusanyika pamoja, tukiwa hai, na upande huu wa Umilele asubuhi hii, na tunaweza kumwabudu Bwana tena, na kukusanyika pamoja na kusikia kutoka Kwake. Hiyo ndiyo sababu tunakusanyika, ni kwa kusudi hili hasa.

² Sasa, kwa namna fulani nilimvamia Ndugu Neville, bila kutarajiwa, leo hii, kwa sababu ya ndoto fulani niliyopata. Ambayo...Ninaamini katika...mimi...katika ndoto. Ninaamini ya kwamba Mungu hushughulika na watu kwa njia ya ndoto. Nami nilipata ndoto isiyo ya kawaida sana, juzi usiku. Kwamba, nilikuwa nikipita ubavuni mwa kilima, ubavuni mwa kilima fulani, nikienda kwenye mkahawa fulani ambapo nilikuwa nile chakula cha—changu cha jioni. Nami nikaona ya kwamba, nilipokaribia mahali pale, walikuwa wakipiga muziki, okestra ilikuwa ikipiga muziki, kwa fidla, na kuwatumbuiza watu wakati wakila. Na kulikuwako na jambo fulani kuuhusu ambalo halikunipendeza, kwa hiyo nikapita tu kitu hicho. Ndipo nikakutana na mtu mmoja akikwea kilima. Nami nikaangalia, na watu wengi walikuwa wakikwea kilima hicho wakielekea kwenye mkahawa huu. Lakini kwa namna fulani niliwaondokea, nikageuka upande wa kulia, ama, wa kushoto.

³ Na kwa namna fulani, huko chini bondeni, ningeweza kuiona maskani. Nikaisikia sauti ya mtu fulani, ikasema, “Mlaki Ndugu Branham kwenye njia panda fulani-fulani. Yeye anashuka kwenye kilima kile pale juu. Na umwambie jambo fulani-fulani.” Ndipo nikafanya hima kufika kwenye hiyo njia panda.

⁴ Ndipo wakati mtu huyo alipokuja, ilikuwa ni Ndugu Neville amevaa suti yake ya hudhurungi, alionekana kama tu vile anavyoonekana ameketi pale asubuhi ya leo. Ndipo akasema, “Ndugu Branham, kama utakuwako humu mjini,” kasema, “lingekuwa ni jambo zu—zuri kwako kushuka uje, kwa maana Ndugu Hank...” Sasa, yule pekee nimjuaye, Ndugu Hank, ni Ndugu Henry Carlson, tunamwita Hank. Kasema, “Huenda akawazia lilikuwa ni jambo lisilo kawaida kwamba

hukuitembelea maskani zaidi kama utakuwako huku mjini, ama humu jijini kwa siku chache.” Nikaamka.

⁵ Na, kwa jambo hilo, kwa namna fulani nilijisikia visivyo kawaida. Sikutaka kuvamia katika wakati huo wa juma, mpaka nilipomuuliza Ndugu Neville iwapo alikuwa na jambo lolote maalum kwa ajili ya asubuhi hii, kwa ajili ya kanisa. Kwa hiyo alikuwa na fadhili, kama kawaida, kasema, “Njoo huku chini.” Kwa hiyo, tumekuja tu. Nilimpigia simu karibu mwisho wa alasiri jana, ndipo nikaja asubuhi ya leo, pasipo kutarajiwa na yeyote wetu.

⁶ Sasa ninaamini ya kwamba lingekuwa ni jambo jema, kwanza, kwangu mimi kwa namna fulani ku—kuwaelezeni mambo fulani. Mimi, inadhaniwa, ni mtu wa kipekee sana kwa watu wengi. Nami kwa namna fulani ni wa kipekee kwangu mimi mwenyewe, pia. Kwa sababu, mimi hujaribu kuufuata uongozi wa Roho Mtakatifu, kwa karibu tu niwezavyo. Na hilo hutufanya wa kipekee, mnaona. Tunafanya mambo ambayo kweli tu—tunaketi chini na kushangaa wakati mwingine, “Ni kwa nini nikafanya jambo kama hilo? Nilipataje kamwe kufanya jambo kama hilo?” Na papo hapo huenda ukafikiri ya kwamba umefanya kile hasa hukupaswa kufanya. Lakini kama utakuwa tu na subira, na uwe na imani, nawe una hakika ya kwamba Mungu amekuongoza kulifanya, utakuta kwamba linafanya kazi vizuri kabisa. Unaona? Na mara nyingi tunaona jambo hilo. Nami ninajua Ndugu Neville ameliona hilo, mara nyingi. Nao viongozi na watu wa kiroho wanatambua hilo.

⁷ Imekuwa wakati mwingine maishani mwangu kwamba... Kusema kweli, tangu nilipokuwa tu mvulana, kamwe sijasikia kuongozwa hasa kwamba inanipasa kuishi Je—Jeffersonville. Daima imekuwa ni kero, kwangu kujaribu kuishi hapa. Jambo la kwanza, hali ya hewa hainifai kabisa. Jambo lingine, inaonekana kuna kukandamizwa kwa roho.

⁸ Ukirejea nyuma na kuangalia mahali fulani hapa, kama haikuharibiwa katika wakati ule wa mafuriko, kuna barua kuhusu hilo, niliyokuwa nayo, nilipoitwa hudumani kwa mara ya kwanza, nilianza kuondoka. Na mimi pamoja na Ndugu George DeArk...

⁹ Na mama yake Ndugu Graham Snelling, Ndugu Hawkins ambaye anaendesha kituo cha petroli huko New Albany, na watu wengine wengi, walikutana nami nje ya mahali padogo pa mkutano wa maombi huku. Na hata wakasema, kama ningekaa, wangewapunguzia watoto wao chakula mezani, ku—kuijenga maskani, kusudi isiwalazimu kuchukuliwa mahali mahali.

¹⁰ Nilipomsikia maskini mama huyo, akiwa amemshika mtoto mmoja kwa mkono wake na huyo mwingine karibu na bega lake, akisema angekuwa radhi kuwapunguzia chakula watoto wake mezani, kusudi wajenge mahali ambapo wangeweza kukaa na

kuabudia, kidogo ilikuwa ni vigumu kwangu kustahimili. Kwa hiyo mimi na Ndugu George tukaungana na kuamua tungekaa na kuijenga maskani.

¹¹ Ndipo wakati maskani ilipojengwa, ilionekana siku zote . . . Ile asubuhi niliyoiweka wakfu maskani, ono lilitokea, ambalo limeandikwa na limo mle kwenye jiwe la pembeni, wakati Roho Mtakatifu aliponiambia, “Hii siyo maskani yako.” Mnaona? Basi nikauliza mahali maskani yangu ilipokuwa, ndipo Yeye akaniketisha chini ya mbingu angavu za bluu. Na kisha akasema, “Fanya kazi ya mwinjilisti,” na kadhalika, kama mjuavyo. Imeandikwa hata kwenye vitabu.

¹² Mambo hayo yote yamewekwa pamoja. Ndipo siku moja wakati nilipokuwa nikikata nyasi uani kule juu ambako Ndugu Wood anaishi sasa, naye mama mkwe wangu aliishi kule wakati huo; niliketi kwenye kipandio cha nyuma, kipandio kidogo cha kale cha saruji, ambapo nilikuwa nimepajenga mahali hapa padogo kwa ajili ya mama mkwe wangu. Naye kwa namna fulani alikuwa ni bawabu wa kanisa wakati huo, akilishughulikia. Na kwa udhahiri tu kama mtu yeyote angaliweza kunena, Sauti ilinena nami, ikasema, “Kamwe siwezi kukubariki mradi tu unakaa hapa. Huna budi kujitenga na watu wako pamoja na mahali hapa.” Vema, mimi, hilo lilinisumbua sana, kwa karibu juma moja ama zaidi.

¹³ Daima, wakati wote, kitu Fulani kimenionya, “Ondoka, ondoka. Elekea upande wa magharibi. Endelea kwenda magharibi.” Vema, mimi . . . Daima limenisumbua. Na inaonekana kana kwamba kila wakati . . .

¹⁴ Sasa, nilikuwa nimeamua wazi niani mwangu ya kwamba juma hili niruke kwa ndege hadi Tucson, ambako nilikuwa nikodi mahali, niwe huko kwenye msimu huu wa baridi kali; kuwapeleka watoto shuleni, kuanzia Septemba. Nilipapata mahali hapo. Hata kulikuwako na mahali nilipopewa kule. Lakini kuna kitu ambacho . . . Na—na kama nimeondoka . . .

¹⁵ Jambo lingine ningetaka kusema. Kabla tu hatujajenga nyumba hii hapa juu, ya mchungaji, mahali ilipo sasa, sikutaka kujenga pale. Mama yake mke wangu alikuwa amezeeka. Na hata alilia kuhusu jambo hilo, akasema, “Kamwe siwezi kumwacha mama hapa, huku nikijua yeye ni mzee, na huenda asihudumiwe.” Vema, nilielewa hilo. Ninaelewa. Huyo ni mama yake, na ndiye mama pekee aliyepata kuwa naye, ama atakayepata kuwa naye. Kwa hiyo, nilielewa hilo. Kwa hiyo ni—nikamwomba Bwana, nikasema, “Bwana, kwa kuwa sipapendi mahali hapa,” nikasema, “nifanye niridhike. Nitaenda mahali popote unaponitaka niende, kutoka mahali popote. Bali sitaki kumhuzunisha mke wangu, kumwondoa hapa, nimpeleke nchi ya kigeni ambako hamjui mtu yeyote. Halafu mimi huwa safarini

wakati wote, hata hivyo. Nifanye tu niridhike kuwa hapa pamoja naye.”

¹⁶ Na sasa, wakati mama yake amechukuliwa, naye ameenda Utukufuni, basi hii hapa hiyo shauku inakuja tena, mnaona, sasa ya kuhama. Sijui la kufanya.

¹⁷ Na basi hivi majuzi wakati fundisho hili ambalo ndugu walikuwa wamelianzisha huku, nilisimama kutoka mimbarani mara ya mwisho nilipokuwa hapa na kuwaambia ya kwamba nisingekuwa hudumani mradi tu hilo lilikuwa linaendelea. Kwa hiyo, hao ndugu kwa rehema walilinyosha hilo lote. Lote limekwisha. Katika muda wa saa ishirini na nne, lilikuwa limekwisha.

¹⁸ Sasa hilo linanifungulia uwanja tena. Sijui la kufanya. Sijui nigeukie upande gani. Nimemwomba Bwana anipe ono. Nimemwomba aniambie la kufanya. Bali ananiacha tu niketi.

¹⁹ Sasa, jana usiku wakati nilipowaondoa watoto wote, mke wangu na wote hao, kutoka nyumbani, nilimtolea Bwana Mungu ahadi. Ndipo nikamwambia Bwana Mungu, “Kama utanibariki katika njia niendayo, nitakutumikia. Lakini itakubidi kunionyesha mahali pa kwenda, na jinsi ya kwenda, na jambo la kufanya.” Kwa hiyo, nikajikabidhi kwa Bwana. Pamoja na—pamoja na huduma na yote, nilikabidhi kwa Bwana. Nami nikasema, “Popote utakapofungua Wewe, chochote ufanyacho, nitatembea katika njia hiyo. Mpaka utakapofanya njia, nitaendelea tu jinsi nilivyo mpaka utakapofanya njia.” Nami nikamwomba aifanye dhahiri sana hata sitadanganyika basi, kwa kuwa kweli ninaamini tuko kwenye njia panda za jambo fulani kutukia.

²⁰ Nilisikia likitabiriwa asubuhi ya leo hapa na Ndugu Neville, ama alilitoa ambapo nilijua lilikuwa—lilikuwa ni unabii aliokuwa akiurejea. Sasa, kwa hiyo, nimewaombea ninyi nyote, nami nawatakeni nyote mniombee, ili kwamba Roho Mtakatifu ataniongoza mahali hasa ninapopaswa kwenda, yale ninayopaswa kufanya, kusudi nisifanye kosa lolote.

²¹ Mnaona, mara nyingi, watu wanafikiri ya kwamba karama ya unabii, kwamba Mungu husema tu “Nitakuchukua papa *hapa*, na kukuweka *hapa* chini. Sasa wewe nenda moja kwa moja *hapa*.” Naye hakwambii mambo hayo yote. Kama angekwambia, basi wewe ulikuwa na imani gani ya ushindi? Unaona? Unaona, wewe, Yeye hukuacha usimame peke yako kuliko mtu mwingine yeyote. Unaona? Ninyi nyote mnaweza kunijia na kuniomba mambo fulani, na Yeye kamwe hajashindwa bado ila amewapa jibu. Hiyo ni kweli. Naam. Lakini mimi ninaweza kumwomba mambo yangu ya binafsi, na mara nyingi Yeye huniacha tu peke yangu, mnaona, ananiacha tu niendeleo na kuingia humo.

²² Nina mambo sasa ambayo inanibidi kuyatatua mwenyewe, na maamuzi yanayonibidi kufanya. Na hili ni muhimu sana,

mpaka siwezi kulifanya mpaka niwe na hakika ya kwamba ni Yeye anayesema na mimi. Na mimi—mimi . . . Yeye hatanipa ono. Ananiacha tu peke yangu. Kwa hiyo nimekaa tu kama yatima, kitu kama hicho, asubuhi ya leo, si—sijui nielekee wapi. Kwa hiyo, nimelikabidhi kwa Bwana.

²³ Ni—nilijisikia kwamba basi, katika kuota hivyo, inanibidi kurudi hapa maskanini na kumsaidia Ndugu Neville mpaka jambo lingine litakapotukia safarini. Kwa hiyo, nitakuwapo.

²⁴ Nilimuuliza Ndugu Neville muda mfupi uliopita, “Kanisa lilikuwa likiendeleaje?”

Naye akasema, “Vizuri.”

²⁵ Na kwa hiyo ninasikia ya kwamba mngali mna karama za kiroho na kadhalika miongoni mwenu, ambazo zinafanya kazi, karama za unabii, na—na kunena kwa lugha, na kufasiriwa kwa lugha, ambako ndio kwanza tusikie muda mfupi uliopita. Na mambo hayo yanalienga kanisa, tena sana.

²⁶ Lakini nilifikiri, labda usiku wa leo huenda mimi, kama Ndugu Neville . . . Iwapo Roho Mtakatifu hatatuongoza kwenye jambo lingine tofauti, usiku wa leo ningetaka kuwa na . . . Ninyi nyote, kabla hamjaondoka asubuhi hii, mjiandikie swali na kuliacha hapa, swali fulani moyoni mwenu, kusudi tupate kujua kile kanisa linachowazia. Karibu hiyo ndiyo njia waliyo nayo wachungaji ya kutafuta kujua kile kilichoko moyoni mwa watu. Na kila mmoja wenu aliye na swali, liandike na uliweke hapa juu. Kama huna kipande cha karatasi cha—cha kuliandikia asubuhi ya leo, basi liandike usiku wa leo, mapema. Kwa hiyo, ningetaka kuwa na wakati mwingi niwezao, juu ya hayo, kuyachunguza na kuwajibu Kimaandiko.

²⁷ Halafu Bwana akipenda, kama yakiwa ni mapenzi ya Mungu; nimetoa tamshi hapa si muda mrefu uliopita, kwamba ningetaka kuwazungumzia juu ya ile Mihuri saba ya mwisho ya ninii . . . ya Ufunuo. Sasa kama tukininii . . . Nisingeweza kuipitia hiyo Mihuri yote mwaka huu, kwa kuwa inachukua kutoka mlango wa 6 wa Ufunuo, hadi—hadi mlango wa 19, kuimalizia Mihuri hiyo. Lakini ile mitatu ama minne ya kwanza ingeweza kujibiwa katika usiku mmoja, nafikiri, kila Muhuri ukichukua usiku mmoja.

²⁸ Sasa, kama tunaielewa, tazama mahali tunapokomea kwenye Kitabu hicho cha Ufunuo, ambapo Kanisa lilitwaliwa juu Utukufuni. Halafu hayo mengine yanashughulika na Wayahudi, sio Kanisa hata kidogo. Yanalishughulikia taifa la Kiyahudi. Kwa hiyo hatuna budi kushuka tena chini, kutoka kwenye kule Kunyakuliwa kwa Kanisa, na kuchukua . . . Tunaona hapa yanayotukia wakati wa Mihuri hiyo, na wakati wa Kanisa la Kimataifa. Kanisa likiisha kuondoka; na pamoja na taifa la Israeli, linashuka na kurejea nyuma na kuwaleta Israeli kutoka

wakati lilipowaacha, kufikia wakati wa sasa; na Masihi ajaye, wakati watakapompokea Masihi.

²⁹ Sasa mnalipata? Kanisa linatwaliwa juu. Mungu alilishughulikia Kanisa kwanza, Nyakati za Kanisa. Tulizichukua hizo. Halafu Kanisa linatwaliwa juu Utukufuni. Ndipo Roho Mtakatifu anarudi na kuwachukua Israeli, kama taifa. Na kuwaleta umbali huu, wakati ile Karamu ya Arusi ikiendelea, kisha anawarudisha tena mwishoni mwa wakati huo. Nitausimamisha ubao wangu, niweze kuichora na kuifundisha, wakati huo utakapowadia. Ndipo Bwana anarudi pamoja na Bibi-arusi, nao Israeli wanamwona. Na, loo, huo utakuwa ni wakati wa jinsi gani!

³⁰ Sasa, kabla hatujalifunga hili kwa usahihi, kuna somo kubwa ambalo ni kikwazo kwa wanatheolojia na waalimu wengi kote katika wakati, na watu wa Church of Christ na wale wanaokuja kulisikia hili, hilo ni, yale Majuma Sabini ya Danieli. Tunaninii. . . Hatuwezi kuendelea mbele katika Ufunuo mpaka tutakapomfunganisha Bibi-arusi na Israeli pamoja na yale Majuma Sabini ya Danieli. Na labda, Mungu akipenda, ili kwamba kama akizungumza nami katika siku za usoni, kuzungumza juu ya baadhi ya haya Majuma Sabini. . . ama, sio Majuma Sabini, bali Mihuri saba ya mwisho. Basi Jumapili ijayo, nitajaribu kuyachukua Majuma Sabini ya Danieli, Jumapili ijayo, Bwana akipenda. Na kisha hayo yatafungua milango basi, kama Yeye akituongoza, kuanza na hayo mengine. Vema, tutaona kutoka hapo na kuendelea.

³¹ Mimi pamoja na Ndugu Neville tutafanya kazi pamoja juu ya jambo hili, na kufanya kila kitu tuwezacho kwa manufaa ya watu.

³² Sasa, tukirudi nyuma kila wakati, tunawaomba wagonjwa, daima tuna furaha kufanya hivyo. Na labda nitafanya hivyo katika kila mkutano, kama watu ni wagonjwa, kuwaomba.

³³ Sina hamu ya kufanya upambanuzi wowote zaidi. Mnaona, sasa hili hapa lililotukia. Nimejaribu. Nami ninajua nimefanya mambo ambayo ni makosa; bali nimejaribu kuishi karibu na Mungu vya kutosha, wakati wote, kwa Mungu, hivyo ndivyo maono haya yangetukia, jinsi ambavyo yangetukia. Hata watu wangepoteza vitu, nao wananiita, wananisihi niwaombee kwa Bwana, kuulizia mahali kilipokuwa. Kama vile Yese alivyowapoteza wale nyumbu, nao wale vijana wakashuka wakaenda kumtafuta nabii, naye akawaambia ambapo hao nyumbu walikuwa tayari wamerudi nyumbani. Kadhalika namna hiyo, hilo ni sawa kabisa. Lakini linazidi sana, watu wengi sana. . . Sio tu katika eneo kama hili; ni kote ulimwenguni, mnaona. Kwa hiyo inakuwa tu, linanitatiza sana, halafu linakutia wasiwasi wakati wote, mpaka inafikia mahali. . .

³⁴ Na hiyo ndiyo iliyowafanya hao ndugu kuanzisha hilo fundisho, ya kwamba nilikuwa Bwana Yesu Kristo aliyefanyika mwili. Nasi tunajua ya kwamba hilo lingeirarua Huduma hii yote vipande-vipande, na kuleta dhihaka juu ya Kristo na kila kitu. Mnaona? Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu ilinibidi kuwatikisa vikali, waliache mara moja, kuwafanya wajue ya kwamba hilo halikuwa ni la Mungu, hilo lilikuwa ni la ibilisi. Mnaona? Nao ni watu wazuri. Na ilionyesha watu hao wamezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, kwa sababu, walipoiona Kweli kwa Maandiko, walimrudia Mungu, hakika, mnaona, mara moja. Kwa hiyo, hiyo ilionyesha ilikuwa ni Shetani akijaribu kufanya jambo fulani na hao watu; wote walikuwa ni wataua, watu Wakristo.

³⁵ Na ili wafanya wengi wao kuniambia, “Ndugu Branham, tuna imani zaidi na wewe sasa kuliko tulivyopata kuwa nayo.”

³⁶ Maana, mnaona ni nini, kwa karama ambayo Mungu amenipa, ningaliweza kufanya nini na hiyo? Kulitupa taifa miguuni pangu, ama, watu. Kile tunachoita *taifa*, siyo “ulimwengu” hapa nje, kile—kile chakula cha mizinga na kadhalika. Ninamaanisha Wakristo, mwaminio halisi, hao ndio walio bora kuliko wote wa ninii. . . Tunazungumza juu ya *taifa*, tunahubiri juu ya “watu waliozaliwa mara ya pili,” hao ndio tunaonena habari zao, taifa. Si kila mtu tu hapa nje, ambao ni wachafu sana na vinyaa ambao tunaishi ulimwenguni, hao ni—hao ni mavumbi tu ya duniani yanayorudi. Ninanena juu ya Wakristo waliozaliwa mara ya pili, watu ambao ni Wakristo halisi.

³⁷ Ninamngojea mtu fulani anirukie tena kuhusu jambo fulani. Mtu mmoja alinjia sio muda mrefu uliopita, na kusema, “Wazo lenyewe, la Kristo akitema mate ardhini, kwa mate Yake, na kufanya tope na kulipaka machoni mwa mtu fulani.” Kasema, “Huo ulikuwa ni uchafu, kinyaa jinsi gani, Kwake kutema mate, kwa mate yake kutoka kinywani Mwake! Ilikuwa ni kukosa usafi jinsi gani, kutema mate ardhini, na kufanya malundo ya matope na kuyapaka machoni mwa mtu.”

Nikasema, “Lakini alirudi akiona.” Unaona, jambo ndilo hilo.

³⁸ Naye mtu yuyo huyo! Walifungua kambi ya wenda uchi huko juu karibu na kwangu, mwajua, kidimbwi cha kuogelea. Na—na mtu huyo anayo tiketi kwa ajili ya kila mmoja wa watoto wake waende kule na kuogelea kwenye kidimbwi kile. Naye na mke wake huenda, pia, kwenye kidimbwi hicho. Mniwie radhi, dada zangu. Lakini ambapo hao wanawake mle ndani wakiogelea, karibu mia moja, ama mia mbili, kila siku; wanawake, uchafu huo wote na kadhalika, na wanawake siku hizi, na wakiogea mle katika hayo maji, uchafu huo na kinyaa vinywani mwao, na kuyameza na kuyatema. Ninamtaka tu anirukie, unaona.

³⁹ Wao walisema, “Kama—kama Kristo alikuwa akiishi leo hii, wangemtia mbaroni kwa sababu ya jambo hilo la kukiuka kanuni za afya.”

⁴⁰ Na *hilo* je? Nina hakika mnashika ninayomaanisha. Wanaingia moja kwa moja katika hicho kidimbwi, na wengi wao wakiwa na magonjwa, wana kaswende, kisonono, na mengineyo yote, moja kwa moja mle ndani. Nawe unayatema tu kwa kinywa chako, na kila kitu namna hiyo, na kuoga mle ndani namna hiyo. Na hiyo ati ni afya, hakika?

⁴¹ Kwa hiyo, loo, jamani, siku hii tunayoishi, ndugu, dada! Wakati wa kule Kuja kwa Bwana umewadia! Nalo Kanisa lina tumaini moja, na hilo ni kule Kuja kwa Bwana.

⁴² Vema, siwezi kuyakomesha mambo hayo; hakuna haja. Biblia ilikwishatabiri yangukwapo hapa. Siwezi kuyakomesha. Bali ninataka sauti yangu iwe kwenye kumbukumbu Mbinguni, ya kwamba niliyapinga, wakati wa ile Hukumu utakapofika. Niliyapinga.

⁴³ Ningali ninaamini ya kwamba Biblia hii ni Neno la Mungu. Basi hakuna kitu kingine ulimwenguni, kinyume Chake, kinachoweza kuikomesha. Lakini hii Biblia hapa, hii ndiyo Kweli, hii ni Neno la Mungu. Kwa hiyo sasa na tutweke matanga ye—ye—yetu, na tutie nanga kidogo kwenye pwani iliyotulia ya Mahali pa Raha. Na—nasi tunaweza kuabiri kesho mahali fulani, lakini hebu na tutie nanga sasa na kuisikiliza Sauti ya Baba yetu wa Mbinguni wakati akinena na sisi kupitia kwenye Neno Lake, tunatumaini, leo.

⁴⁴ Na usiku wa leo, sasa, jiandae na swali lolote dogo ulilo nalo. Sasa, si kitu kitakachomdhuru mtu fulani. Kama ukifanya hivyo, basi hiyo ni . . . Nisingejibu hilo, kwanza kabisa, unaona. Lakini wewe, kitu fulani, tuseme, “Vema, sasa, kama nikifanya jambo *fulani*, je! Mungu anasema tunapaswa kufanya jambo hili?” Ama, mwajua, maswali madogo moyoni mwako. Ama, “Tuna karama zinazofanya kazi kwetu, Ndugu Branham, na je! tuzifanyie kazi *hivi* ama *vile*? Ama, tufanye nini?” Jambo fulani ambalo ningeweza kukujibu katika Maandiko, unaona. Andika kitu fulani kidogo. Ningefurahia. Na kama hakuna, basi nitachukua tu somo la namna fulani, na kuwahubiria usiku wa leo, Bwana akipenda. Hii ni Jumapili, nami nimekuwa . . .

⁴⁵ Jumapili iliyopita nilianza kwenda huko kwa Ndugu Cauble. Nami nikasikia kengele ya kanisa hili ikilia, nami nikaenda huku na huko uani. Nisingeweza kuvumilia jambo hilo. Hivyo tu. Niliwasikia, kwa hiyo i—i—ilinibidi tu kushuka kuja hapa.

⁴⁶ Kwa hiyo sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa na kunena na Muumba wetu, na halafu katika maombi madogo. Je! kuna mtu aliye na haja maalum? Inueni tu mikono yenu, msemi tu, “Mimi. . .” Fanyeni tu ijulikane. Mungu anajua kilicho moyoni mwako. Sasa weka tu haja yako niani mwako.

⁴⁷ Mungu aliye Mtakatifu kuliko wote, Ambaye uliziumba Mbingu na nchi kwa Neno la kinywa Chako, kwa mawazo ya moyo Wako. Tunakuja katika Uwepo Wako, kupitia Yesu Kristo, Bwana wetu, kukushukuru kwa ajili ya yote ambayo umetufanyia. Nasi tunakushukuru sana, Bwana, asubuhi ya leo, kujua mahali tunaposimama, kujua nafasi tuliyomo asubuhi ya leo, na historia ya wakati, na mambo ya baadaye yajayo. Tukijua leo hii, ya kwamba kwa neema ya Mungu, ya kwamba tumeoshwa katika Damu ya Kalvari, ya kwamba tumejiandaa, tukiwa na imani mioyoni mwetu, kumlaki Yeye ikiwa angekuja leo hii. Inatupasa kusema, “Hata hivyo, njoo, Bwana Yesu.”

⁴⁸ Nasi tunaona dhambi ikilundikana, mpaka inaonekana kana kwamba ulimwengu unayumbayumba chini ya athari ya dhambi. Jinsi ambavyo kunywa pombe na kucheza kamari, na karamu za ulevi, na uchi, na, Ee Mungu, uchafu, na taka na kinyaa cha watu. Na jinsi ambavyo wao, laiti wangelitambua, Bwana! Je! watu hao, wanaovalia jinsi hiyo katika maskini nguo hizo chafu zisizo za kitauwa, na wanaenda huko nje mtaani, hivi wanatambua ya kwamba wao si kitu ila wadudu na mavumbi, ambao labda katika juma lingine wadudu watakuwa wakiula huo mwili ambao wanautukuza jinsi hiyo? Hivi wanatambua ya kwamba parare wataula? Nayo nafsi yao itakuwa huko ng’ambo katika Umilele bila ya Mungu, bila ya Kristo, bila ya tumaini, ikitumbukia ndani kabisa katika kufa moyo, wapate kuangamizwa kabisa katika Kuja Kwake. Ee Mungu, tupe sauti za—za maonyo, tupate kumwonya kila mtu juu ya hatari hii wanayoikaribia.

⁴⁹ Uwe pamoja nasi leo hii. Tupe “maneno ya hekima,” kama vile Sulemani alivyosema wakati mmoja katika Mhubiri, tuweze kuwa “wajenzi wenye hekima,” tupate kuwa “wachungaji wa kusanyiko hili.” Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba tunapoyatafuta maneno ya kusema, ya kwamba yapate kuwa—yapate kuwa ni vipeo ambavyo vingeanasa moyo ulio na haja sana hapa asubuhi ya leo.

⁵⁰ Hatujaja na kukusanyika chini ya paa hili lenye joto leo hii, tupate tu kuonekana, bali tumekuja hapa kwa sababu tunakupenda, na kwa sababu tunatamani kusikia kutoka Kwako. Wewe ni Mpenzi wetu tunayempenda, nasi tunatamani kusikia Maneno kutoka Kwako. Tunashukuru kwa ajili ya yale tuliyokwisha kusikia. Yatadumu pamoja nasi kwa muda mrefu. Sasa tupe sehemu uliyo nayo kwa ajili yetu leo, tunapoendelea kukungojea Wewe. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

⁵¹ Sasa ni...[Dada mmoja ananena kwa lugha nyingine. Ndugu mmoja anatoa tafsiri yake—Mh.]

⁵² Tunashukuru kwa ajili ya huku kutukuzwa kutoka kwa Roho, kunatwambia na kutuonya tuyaangalie Maneno ambayo

labda Roho Mtakatifu atatuzungumzia leo. Nasi hatujui ni kitu gani alichotuwekea akiba, bali tunajua ya kwamba hapana budi kuna kitu fulani atakachotoa. Labda swali limo moyoni mwako, kwamba atalinena kupitia hapo. Huenda akalinena kupitia kwenye Ujumbe asubuhi ya leo. Huenda akalinena usiku wa leo ibadani. Yeye, wakati fulani leo hii, Yeye anajaribu, inaonekana kama, kumwonya mtu fulani ayashike Maneno hayo.

⁵³ Sasa kuligeukia Neno lililoandikwa, hebu twende kwenye Kitabu cha Kutoka, kwa ajili ya somo la Shule ya Jumapili.

⁵⁴ Je! mna ibada ya ubatizo? [Ndugu Neville anasema, “La, hatuna mpaka saa kumi na mbili jioni ya leo.”—Mh.] La. Ibada ya ubatizo kwenye saa kumi na mbili alasiri ya leo.

⁵⁵ Hebu twende kwenye mlango wa 17 wa Kutoka, na tuanzie kwenye—kwenye kifungu cha 5, ninaamini, kifungu cha 5 na cha 6 cha mlango wa 17 wa Kutoka.

BWANA akamwambia Musa, Pita mbele ya watu, ukawachukue baadhi ya wazee wa Israeli pamoja nawe; na ile fimbo yako ambayo uliupiga mto kwayo, uitwae mkononi mwako, ukaende.

Tazama, nitasimama mbele yako...juu ya ule mwamba huko Horebu; na...utaupiga mwamba, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli.

⁵⁶ Sasa kama ningeliita hili somo dogo la Shule ya Jumapili, ningetaka kuchukua hili kama somo la asubuhi ya leo, *Maji Yaliyopo Daima Yatokayo Mwambani*.

⁵⁷ Tunajua ya kwamba Israeli daima imekuwa ni mfano wa kihistoria wa kanisa. Maana, Israeli ilikuwa ni watu wa Mungu mpaka walipotoka Misri, na ndipo walikuwa ni kanisa la Mungu kwa kuwa walikuwa wametenganishwa na walimwengu wengine.

⁵⁸ Na sisi tunapotenganishwa na walimwengu wengine, ndipo tunakuwa ni kanisa. Lakini mradi tumejizonga na walimwengu wengine, basi hatuko kwenye kanisa. Sasa natumaini kwamba hilo linaingia ndani kabisa, linashika mahali pake. Mnaona, sisi sio kanisa mpaka tumetenganishwa na ulimwengu. Kujitenga wenyewe, kutoka miongoni mwa watu wachafu, tusiwe na uhusiano nao, wala tusizishiriki dhambi zao. Usifungwe nira pamoja na wasioamini, bali jitenge na mambo ya ulimwengu.

⁵⁹ Na wakati Israeli walipokuwa Misri, walikuwa ni watu wa Mungu. Ndipo wakati walipoitwa watoke, ama walipokuwa na kule kutoka, wakitoka nje, basi waliitwa kanisa, kwa sababu hapo ndipo walipojitenga wenyewe na walimwengu wengine.

⁶⁰ Nalo neno lenyewe *kanisa* linamaanisha “walioitwa watoke.” *Kutoka*, “kutoka nje.” Kila mmoja wetu, kama Wakristo, amekuwa na kutoka maishani mwetu. Tulikuwa

na wakati ambapo tuliitwa tutoke miongoni mwa wenzetu, tukaitwa tutoke miongoni mwa watu ambao wakati mmoja tulishirikiana nao, na tukawa watu tofauti, kutembea pamoja na watu tofauti waliotenda tofauti na kuzungumza kwa njia tofauti. Ilikuwa ni kutoka katika maisha yetu.

⁶¹ Mfano mzuri sana ambao Israeli ilitupa, wa wakati ambapo Mungu aliwaita watoke. Walikuwa na kutoka, nao wakatoka miongoni mwa wa—watu wa ulimwengu, wakawa taifa lililotengwa, kwa Mungu, watu wa kipekee. Walitembea chini ya vivuli vya kiti cha rehema. Waliishi na kutembea kwa ile Nguzo kuu ya Moto. Naye Mungu akawatoa Misri, akawapeleka kwenye nchi aliyoahidi.

⁶² Na, katika kutoka huku, walipewa kiongozi wa kiroho, kiongozi, ambaye alikuwa ni Musa, nabii mkuu aliyetiwa mafuta ambaye alikuwa ni mtu m—mkuu. Alikuwa ni mtu mtauwa, alizaliwa mtu mtauwa. Mungu alimwita kutoka kwa mama yake, hata kabla ya wakati huo; Mungu alimchagua kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu, apate kuwa kiongozi wa kizazi hicho, kuleta huku kutoka kwa watu.

⁶³ Hapa wakati fulani uliopita, nilizungumza na watoto wadogo hapa maskanini, nami nilikuwa na mahubiri madogo kwa ajili yao; na kuwaambia, ama kutoa mfano mdogo wa jinsi ambavyo Yokebedi, jinsi alivyoomba, yeye na Amramu, baba yake Musa, kuhusu kufanya jambo fulani kuhusu kuwakomboa watu hao. Ndipo Amramu akaona ono la Mungu amesimama, ama Malaika, akielekeza kaskazini, na akamwambia kile ambacho kingetukia. Ndipo maskini mtoto Musa akazaliwa. Nao hawakuogopa amri za mfalme, wala vitisho vyake. Walijua kwamba Mungu alikuwa ameweka mkono wake juu ya Musa, na hilo lilitosha. Hiyo ni kweli. Haijalishi mfalme alisema nini, kile ulimwengu wa kisiasa ulichosema, kile kitu kingine chochote kilichosema, wao walijua Mungu alikuwa ameweka mkono Wake juu ya Musa. Kwa hiyo hawakuogopa kumwachilia, moja kwa moja katikati ya mamba; wakati wote walipokuwa wamenona kwa watoto wa Kiebrania, ambapo walikuwa wamewatoa kule wakaliwa na mamba. Na hata hivyo Musa aliwekwa moja kwa moja ndani ya kijisafina kidogo na kupelekwa huko nje moja kwa moja miongoni mwa hao mamba, moja kwa moja kati yao. Kwa sababu, hawakuogopa kitu, walijua kwamba Mungu alikuwa ameweka mkono Wake juu ya Musa.

⁶⁴ Vema, sasa, kama tungeweza tu kujua jambo lilo hilo, ya kwamba Kiongozi wetu mkuu, Roho Mtakatifu, Mungu amentuma. Naye Ndiye kiongozi wetu. Na haidhuru ulimwengu unasema nini, na kwamba wanawacheka kiasi gani na kuwadhihaki, sisi tunamfuata Kiongozi wetu! Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kuwa Kiongozi wetu. Mnaona? “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena. Bali ninyi

mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Kwa hiyo, Kiongozi wetu mkuu yuko pamoja nasi, Roho Mtakatifu. Sasa lazima tumfuate Kiongozi huyu na kufanya yale hasa anayosema tufanye. Naye Kiongozi huyu kamwe hatatuondoa njiani, Yeye atatuweka moja kwa moja kwenye njia ya Maandiko wakati wote. Bali kamwe hataenda upande *mmoja* kwa jambo fulani, na upande *huu* kwa jambo fulani. Yeye atadumu moja kwa moja kwenye barabara ya Maandiko.

⁶⁵ Naye Musa alikuwa na njia aliyokuwa awapitishe Israeli, na waifuate moja kwa moja waivuke Bahari ya Shamu, moja kwa moja wauvuke Yordani, waingie moja kwa moja katika nchi ya ahadi, moja kwa moja kupitia jangwani. Musa siye aliyeondoka njiani. Mungu siye aliyeondoka njiani. Watu ndio waliotoka njiani, ndio waliosababisha ile taabu. Kwa hiyo, hebu na tuyawazie mambo haya sasa. (Samahani.)

⁶⁶ Musa, kama kiongozi aliyetiwa mafuta. Hatimaye, alipokwisha kuwaonyesha hao watu, kwa ishara na maajabu, ambayo Mungu peke yake Ndiye angaliweza kuyafanya, alifanya ishara hizi na maajabu mbele ya wazee wa Israeli, na mbele ya Israeli, mpaka wakaridhika ya kwamba huyu Musa alikuwa ndiye mtiwa mafuta ambaye alikuwa awatote kwenye nchi hii, awapeleke kwenye ile nchi nzuri ambayo walikuwa wameahidiwa. Ndipo walipoona mambo haya makuu ambayo Musa aliyafanya katika jina la Mungu, walikuwa radhi kumfuata. Ndipo akawatoa, na kuwaongoza kupitia kwenye Bahari ya Shamu, wakaivuka, walikuwa kwenye nchi kavu. Na safari ya kuingia jangwani, ambayo inamaanisha wakati wa majaribu.

⁶⁷ Wakati mtu anapompokea Kristo kama Mwokozi wake, kila kitu kiko juu ya nyumba. Lakini, kabla mtu huyu hajaingia kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu; mtu huyu, hana budi kwanza kuwa na mchakato wa utakaso. Hana budi kuwa na wakati wa kujaribiwa maishani mwake. Ninyi nyote mlikuwa nao. Alikuwa na wakati huu wa majaribu. “Kila mwana amjiaye Mungu, kwanza anateswa, anarudiwa, anaadhibiwa. Na endapo hatuwezi kuyastahimili marudio, basi inaonyesha sisi si wana wa Mungu; tu wanaharamu, wala si wana wa Mungu,” Biblia ilisema. Lakini kama tunaweza kustahimili kurudiwa, tukijua ya kwamba “mambo yote hutenda kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu,” ndipo sisi ni wana na binti za Mungu, ndipo Yeye anatutia muhuri kwa Roho Mtakatifu hata siku ya ukombozi wetu. Mnaona, huko ni kurudiwa, majaribu, jambo tunalopitia.

Nao Israeli, kama mfano wa kihistoria, iliwabidi kuyastahimili marudio haya.

⁶⁸ Sasa, wakati walipokuwa huko chini Misri, ndipo Mungu akamtuma Musa. Basi aliinyosha fimbo, na viroboto na chawa wakaja ardhini. Akainyosha kuelekea kwenye jua, nalo likatua. Akainyosha juu ya maji, nayo yakageuka yakawa damu. Mbona, Waisraeli walikuwa huko Kanaani...huko katika—katika Gosheni, wakiwa tu na wakati mzuri; jua kamwe halikutua, mapigo kamwe hayakuwapiga; mbona, walikuwa tu na wakati mzuri!

⁶⁹ Ni kama tu ulivyofanya wewe wakati ulipookolewa kwa mara ya kwanza. Kila kitu, ndege waliimba tofauti, na kila mtu alikuwa ni mzuri sana. Na, loo, jamani, jinsi ambavyo kila kitu kilikuwa ni kizuri sana tu wakati ulipookolewa kwa mara ya kwanza! Ndipo ukaja wakati wa majaribu, kurudiwa, wakati wa kutakaswa, kujitakasa na mambo ya ulimwengu, “ukiweka kando mizigo ikuzingayo kwa upesi.” Wewe, mwanamume, ilikubidi kuacha uvutaji wako wa sigara, kuacha unywaji wako wa pombe, kuacha kwenda kwako kwenye chumba cha kucheza kamari, karamu zako za usiku kucha za kadi. Mambo hayo yote, ilikubidi kujitakasa kutokana nayo, kwa imani katika Damu ya Yesu Kristo. Kujitakasa! Ninyi wanawake iliwabidi kuacha nywele zenu zikue, kuzirefusha nguo zenu, na kutenda tofauti na jinsi mliyokuwa. Wakati wa kutakaswa! Mara nyingi wangeasi na kurudi nyuma; vema, huyo si mwana wa Mungu, mnaona. Mwana wa Mungu huangalia moja kwa moja Kalvari, na anajua kwamba ni kwa ajili ya manufaa yake.

⁷⁰ Kwa hiyo basi kipindi hicho cha wakati, hapo ndipo kule kuanguka kuku kulipokuja, katika Israeli. Hapo wakati huu wa msongamano mkubwa, ndipo watu walipoanza kuanguka, kutoka upande mmoja hadi mwingine. Ndipo katika mazungumzo yao, “Vema, laiti tungalikuwa tumerudi huko Misri. Nafsi zetu zinauchukia mkate huu mwepesi.” Kwa maneno mengine, kama ningelichukua kihistoria sasa, hivyo ndivyo walivyosema.

⁷¹ Sasa katika siku hizi, ingekuwa, “Loo, kila Jumatano usiku, mkutano wa maombi! Kila Jumapili asubuhi, kurudi kanisani! Tunasikia nini? Kitu kile kile; mhubiri anasimama na kuhubiri; nyimbo; endelea kurudi.” Mnaona, basi unaenda tu kama wajibu. Wewe si mwabuduo. Mwabuduo huenda kule kuabudu, kujieleza mbele za Mungu wake, kumsifu Mungu kwa ajili ya wema Wake; kwa kila Neno, yeye anajishikilia Kwalu.

⁷² Ni kama tu mapenzi. Kama ulikuwa ukiandamana na msichana kwa sababu ulijua ilikuwa ni wajibu, ama unaambatana na mvulana, wakati ulipokuwa kijana. “Mama ananitaka niambatane na jamaa huyu, bali hata kamwe siwezi kumvumilia.” Hupati chochote kwake kuja kukuona. Ama, kama ni vile vile kuhusu msichana kwa mvulana, ama mvulana kwa msichana. Unaambatana naye, anakuchosha; mama anakutaka uambatane naye kwa sababu yeye ni aina ya msichana ambaye

mama anampenda. Unaona, inakuchosha; hakuna mapenzi hapo. Lakini wewe hujali, hutaki kuoga, hutaki kwenda kumwona. Nayo ni ninii... Mbona, ni jambo la kuchukiza sana. Na wakati anapokuja kukuona, jamani, unatamani tu angaliondoka upesi, aende zake nyumbani.

⁷³ Hivyo ndivyo ilivyo wakati wewe, “Ni kwa nini yeye anahubiri kwa muda mrefu hivi? Na vipi kuhusu mambo *haya* yote, na kila kitu?” Unaona, wewe huna mapenzi.

⁷⁴ Lakini wakati kweli unapolishikilia kila Neno, kama Roho alivyowapa onyo asubuhi ya leo, mnaona, “Kushikilia kila Neno.” Huenda hilo likawa ndilo ambalo amekuwa akiwazungumzia juu yake. Kushikilia! Ni Uzima wa Milele, kila Neno la Mungu. Ni furaha kwenda kanisani, katika hali yoyote ya mambo. Kama kuna joto, baridi, vuguvugu, kama watu wanazozana, wananung’unika, chochote wanachofanya, ingali ni furaha kulisikia Neno la Bwana. Ndipo unapendana na Kristo basi, unaona, unapenda kwenda kanisani.

⁷⁵ “Vema, mpenzi, hii hapa Jumapili asubuhi tena, ninadhani hatuna budi kuwaogesa watoto na kwenda kule chini. Jamani, inachosha!” Unaona, wewe humpendi.

⁷⁶ Lakini kama kweli unampenda, huwezi tu kungojea hata Jumapili asubuhi ifike, inakubidi tu kushuka kule chini pamoja nao. Nasi tunafika, na kuondoka... Watu wa Mungu, hawakuchoshi. Mbona, wao ni—wao ni ndugu na dada. Kama nilivyozea kusema, “Unakolea kama molasi ya Mtama kwenye asubuhi yenye baridi.” Hai—haitiririki, inakaa tu pamoja, mwajua, inashikana kabisa. Sasa, huo ni msemu jeuri, lakini ni—ni—ni kujaribu kuwajulisha kile ninachomaanisha, mnaona. Mnashikana pamoja. Na kadiri inavyozidi kuwa baridi, ndivyo wanavyoshikana kwa nguvu zaidi. Na hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa kwetu sisi. Kadiri inavyokuwa baridi... .

Marafiki wa duniani wakikuacha,
Bado endelea kushikilia Kwake zaidi.

⁷⁷ Na kile tunachopendana, mmoja kwa mwingine, si kwa sababu sisi ni mtu fulani; bali ni Kristo ndani ya kila mmoja wetu, ndiye tunayempenda, mnaona. Ni yule Mungu aliye ndani ya utu wetu, Ndiye tunayempenda. Sasa tunapenda kukusanyika pamoja. Tulizoea kuuimba ule wimbo wa kale wa kanisa:

Kibarikiwe kifungo kiifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wa nia moja
Ni kama wa huko Juu.

Mnaona, ushirika wa watu wenye nia moja ni kama wa huko Juu.

Mbele ya kiti cha enzi cha Baba yetu,
 Tunamwaga shauku ya maombi yetu;
 Hofu zetu, matumaini yetu, malengo yetu ni
 mamao,
 Faraja zetu na wajibu wetu.

⁷⁸ Mnaona? Naam, bwana! Wakati mtu amekuwa na baraka, sisi sote tuna furaha kuhusu jambo hilo. Wakati mtu mmoja ana huzuni, sote tunahuzunika pamoja naye. Sisi, sisi tunataka kuwa pamoja sote. Sasa hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa.

⁷⁹ Na hivyo ndivyo Israeli walivyopaswa kuwa. Lakini ukawa ni mzigo, “Loo, maskini mkate huu mwepesi, mkate wa Malaika! Vema, tunajali nini kuhusu maskini mkate huu mwepesi? Nafsi zetu zinakichukia kitu hiki! Na kila kitu kimeharibika. Na—na maskini mana hii ya kale inayoshuka kila usiku, mbona, afadhali tule kitunguu saumu na iliki kutoka Misri.” Mnaona, mioyo yao haikuwa tayari kwa safari hiyo.

⁸⁰ Na wakati mwanamume ama mwanamke anapoanza kulalamika juu ya kwenda kanisani, wanachoshwa sana na kwenda kanisani, hawako tayari kwa ajili ya safari. Hiyo ni kweli. Kuna kasoro fulani mahali fulani.

⁸¹ Loo, mnapompenda Mungu, na mkiwazia mnaenda Mbinguni, nanyi nyote mnaenda pamoja!

Ni ushirika wa jinsi gani, ni furaha ya kiungu
 ya jinsi gani,
 Kuegemea kwenye ule Mkono wa milele;
 Loo, ni amani ya heri jinsi gani Bwana wangu
 akiwa karibu hivi,
 Nikiegemea kwenye Mkono Wake wa milele.

Ni ninii . . . Tunaziimba nyimbo hizo.

Tunashiriki ole zetu za pamoja,
 Tunabeba mizigo yetu pamoja;
 Na mara kwa mara mmoja kwa mwingine
 hudondosheana
 Chozi la huruma.

Tunapoachana,
 Inatuumiza kwa ndani;
 Lakini tungali tumeunganishwa moyoni,
 Na kutumaini kukutana tena kwenye wakati
 ujao wa mkutano wa maombi. (Naam,
 bwana, tungali tumeungana moyoni!)

⁸² Sasa mnakuwa tayari kwa ajili ya safari hiyo, mnaona, mko tayari kuingia katika Nchi ya ahadi. Nyakati za majaribu, hilo ndilo eneo la hatari; jangwani, nyakati za majaribu.

⁸³ Israeli, katika wakati wao wa majaribu, walianza kugombana na kuzozana wao kwa wao, wakiuchukia ule mkate. Nao walitaka kurudi Misri.

⁸⁴ Ndipo basi wakaanza kunung'unika juu ya kiongozi wao. Loo, walihofu kwamba alikuwa akiwaongoza vibaya; baada ya yeye kujionyesha kwamba ni kiongozi, na Mungu alikuwa amethibitisha ya kwamba alikuwa ni kiongozi. "Vema, labda kidogo tumefanya kishupavu. Na—na labda tumepotea, sote tukaenda kombo." Ama, kitu kama hicho, mnaona. Walikuwa wakizungumza dhidi ya Mungu na dhidi ya Musa, Mungu na kiongozi Wake.

⁸⁵ Sasa tunapofikia mahali, kusema, "Sijui kama Neno linamaanisha *Hili*, ama siyo. Wala sijui kuhusu Roho Mtakatifu; kidogo nina shaka juu ya Hilo. Ninajua wengine ambao hawana." Vema, endelea uingie Misri. Unaona?

⁸⁶ Lakini kama kweli umedhamiria kukaa barabarani, kaa moja kwa moja na huyu Kiongozi, Roho Mtakatifu, dumu na Neno. Na kama ukidumu na Roho, Yeye atakudumisha kwenye Neno. Hiyo ni kweli. Yeye atakuchukua moja kwa moja barabarani, njia ya Neno. Tena usimwogope. Hataumiza chochote. Atakusaidia tu kama umeumizwa. Atayaponya maumivu yote, Roho Mtakatifu ataponya.

⁸⁷ Sasa tunaona ya kwamba, kwenye njia hii, baada ya wao kuwa jinsi hii, walifikia mahali pa Horebu. Nayo H-o-r-e-b-u, Horebu, basi tunaona. . . Hebu tulichambue jina hilo. Hapo ndipo ji—jina *Horebu* linamaanisha "mahali pakavu" ama "jangwa."

⁸⁸ Na tunapotoka kwenye ushirika mmoja na mwingine kanisani, na kutoka kwenye ushirika na Roho Mtakatifu, inatuleta kwenye mahali pakavu, jangwani, hakuna kilicho hai, kila kitu kina miiba. Mnaona, ja—jangwani, kipande kidogo cha mpungate kikiwa na mwiba. Mlijua hiyo ni nini? Hilo ni jani dogo laini la thamani ambalo halijapata maji, limejisokota tu kabisa hata likawa mwiba. Na unapomwona mtu fulani kama huyu, labda ni nafsi ya thamani ambayo ingelimwagiliwa maji vizuri, ingelikuwa ni jani dogo laini ama chochote kile. Lakini badala yake, limejisokota sana hata likawa ni mwiba, likidunga tu kila kitu, mwajua, likitafuta makosa. Kitu pekee linachohitaji ni maji. Hivyo tu. Linaninii tu linahitaji tu u—uamsho, ama kuvunjika, kuburudishwa kutoka kwa Bwana. Lita—litajifungua lenyewe, kama tu utaliweka kwenye maji.

⁸⁹ Lakini, hapo ndipo ambapo hao wanaoishi mahali hapo inawabidi kuvumilia hali za mahali hapo. Nao wale wanaotamani kuishi katika mazingira ya aina hiyo, ya mahali ambapo kila kitu ni kugonga tu na kuzozana, na kugombana na kushikwa na kiherehere namna hiyo, vema, utaishi tu chini ya mazingira hayo, hivyo tu. Lakini si lazima tuishi mle, haina haja kwetu kuishi mle.

⁹⁰ Sasa, hii Horebu ilikuwa ndipo mahali ambapo Mungu alivunjika moyo kuhusu watu hao, kwa kuwa walikuwa

wamezurura mahali hapa nao wakaingia katika hali hii. Naye akawaleta moja kwa moja kwayo, kwa kuwa wasingetembea kwenye ile njia. Waliondoka kwenye ba—barabara kuu, wakatoka na kuingia kwenye barabara hii ya pembeni. Ndipo ikamfanya Mungu kufanya jambo lililokuwa ni la kuogofya sana. Yeye. . . Ikamfanya Mungu kumwamuru Musa aichukue fimbo ile ya hukumu ambayo alikuwa ameli hukumu taifa kwayo, na kuupiga Mwamba, utoe maji.

⁹¹ Sasa, pana somo zuri hapa kama tungeweza tu kulipata, mnaona. Na kwa sababu tumevurugika sana, na kufungwa na ulimwengu, na kadhalika, ilimfanya Mungu kuzichukua hukumu za ulimwengu na kumpiga Mwanawe Mwenyewe kwazo, pale Kalvari, tupate kuwekwa huru. Mnaona ninalomaanisha?

⁹² Sasa, ili kuwapeleka watu hawa kwenye maji, wakiisha kufika kule, mahali hapa pakavu palifanywa Kalvari. Na hapo Mungu akamwambia Musa, akasema, “Ichukue ile fimbo pamoja na wazee, na mwende mbele, Nami nitasimama juu ya Mwamba mbele zenu.” Nao Mwamba huu ulikuwa ni Kristo. Naye Musa, akiwa na ile fimbo aliyoliletea hukumu taifa la Israeli, alichukua fimbo hiyo hiyo na kuzipiga hukumu za Mungu juu ya huo Mwamba. Unaona? Alizichukua dhambi za watu hao kwenye fimbo hii. Ambapo, ilimpasa kuwapiga watu hao. Badala ya kuwapiga watu hao, yeye aliupiga Mwamba. Nao Mwamba huo, kupitia kazi ya Mungu, ukaleta wokovu, ukaleta maji kwa watu waliokuwa wakiangamia. Ulileta uhai kwa watu waliokuwa wakifa. Na hivyo ndivyo Mungu alivyofanya kwa kuichukua fimbo Ya—Yake rasmi ya hukumu, na kuzizungushia dhambi zangu na zako kwenye fimbo hii; wakati ilipaswa kutupiga, bali ilimpiga Kristo; hata kutoka Kwake yakaja *maji*, ambayo yanamaanisha “Roho,” Roho Mtakatifu akatoka Kwake, ili kutupa Uzima. Sasa tunao Uzima wa Milele. Sasa, Mwamba huu ulikuwa ni Kristo. Sasa tunataka kuona.

⁹³ Nimeona michoro mingi sana ya kiakili ya Mwamba huu. Niliiona moja ya iliyo makinifu sana, si muda mrefu uliopita, hata palikuwapo na mwa—mwamba mdogo uliwekwa juu ya kilima. Na—na Musa alidhaniwa alikuwa ameupiga mwamba huu, nao Israeli walikuwa kule chini wakiwa na kikombe cha chai, wakijipatia maji kutokana na mnyunyizo mdogo ulioanguka kutoka kwenye mwamba huu. Sasa hilo ni wazo tu la mtu fulani.

⁹⁴ Lakini wakati Mwamba huu ulipotoa maji Yake, kulikuwako na zaidi ya watu milioni mbili, mbali na maksai, ngamia, na kila kitu kinginecho kilichokunywa mapipa ya maji kutoka Kwake. Kilikuwa ni kijito kinachobubujika kilichotoka mle!

⁹⁵ Hivyo ndivyo wanavyojaribu kumfanya Kristo, Roho Mtakatifu leo. “Ni mnyunyizo mdogo tu.” Mnaona, wa kutosha tu kukufanya uamini ya kwamba Mungu yupo. La.

⁹⁶ Ni Maji tele! Daudi alisema, “Kikombe changu kinafurika!” Ni bubujiko tu la Roho Mtakatifu.

⁹⁷ Watu wanaliogopa. Watu wengine husema, “Vema, ninahofu tu kidogo nitafanya *hivi* ama *vile*, ama ikitokea kwamba niingie kwenye kilindi kidogo kupita kiasi. Ninaweza kukuonyesha mtu fulani aliyekwenda umbali mrefu kidogo kupita kiasi.” Lakini kamwe huelekezi kwa yule ambaye hakuenda umbali wa kutosha. Unaona? Naam, vipi kuhusu wale ambao hawakuenda umbali wa kutosha?

⁹⁸ Sasa, tumekuwa na baadhi ya watu ambao waliingia katika mwili, nao wakaenda kombo. Na—na si Mungu, bali watu wakaninii. . . Kwa sababu ya ukosefu wa uongozi mwema, na kadhalika, wakaenda kombo, nao wakaingia katika ushupavu wa dini. Ndipo basi ulimwengu mzima, ibilisi anawaelekeza kidole, “Waangalie wale! Waangalie wale!”

⁹⁹ Vema, hebu nisimame asubuhi ya leo na nirejee kwenye hawa makumi ya mamilioni mara nyingi ambao hata hawakuanza safari. Nao je? Mnaona, angalia hali zao. Mwangelie jamaa kama Eichmann leo, akiwa na ya juu kuliko wote. Wao husema, “Wapentekoste hawana maadili na ni washenzi, wala hawana elimu,” na kadhalika namna hiyo. Mwangelieni Eichmann, mmoja wa watu walio na elimu sana ulimwenguni. Naye aliwaua, watoto na wanawake na wanaume milioni sita, nafsi milioni sita. Hutaki kumwelekeza kidole mtu kama huyo.

¹⁰⁰ Lakini maskini mtu mdogo ambaye asingeweza kusoma, ilikuwa ni vigumu kwake, labda alilitamka jina fulani la Biblia vibaya, na, ama labda alisema kitu fulani ama akafanya kitu fulani vibaya, ama akafanya kosa fulani, magazeti yanataka kuliandika kila mahali, na kusema, “Si wa kuaminiwa.”

¹⁰¹ Basi ikiwa hao hawawezi kuaminika, kwa nini si elimu, hayo mambo na wenye akili walio nao leo hii? Mwangelie Adolf Hitler. Waangalie wenye akili wa ulimwengu leo hii. Waangalie. Ule msemo wa kale, “Sheria ni msumeno.”

¹⁰² Jambo unalopaswa kufanya ni kuweza, kwa Roho Mtakatifu, kutenganisha kilicho kweli na uongo, na kuchukua kilicho ukweli na uongo.

¹⁰³ Sasa, tunaona ya kwamba Kalvari hii waliyokuwa nayo, nayo maji ya uzima yakawabubujikia watu.

¹⁰⁴ Sasa, watu wengine wanalo mioyoni na niani mwao, ya kwamba Israeli wote walikunywa, kisha wakawapakia ngamia na kuwafungia farasi wao matandiko, na kadhalika, na kuwachukua watoto wao na kusafiri wakaenda mahali pengine, na kuuacha ule Mwamba pale, ukinyunyiza. Hilo ni kosa.

¹⁰⁵ Huo Mwamba uliwafuata, na hayo maji yaliwafuata. Sasa katika Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 10, ninaamini, na kifungu cha 11, mnaweza kupapata, kwamba, “Mwamba huo uliwafuata Israeli.” Popote walipokwenda tangu siku hiyo na kuendelea, Mwamba huo ulienda pamoja nao, nayo maji hayo yakawafuata.

¹⁰⁶ Ni mfano mzuri jinsi gani, na ngo—ngome nzuri na nanga kwa mwaminio leo hii, anayejua ya kwamba Mwamba huo ambao ulipigwa wakati mmoja, yale Maji ambayo wakati mmoja yalimwagwa kutoka Kalvari, yanaambatana nasi popote tulipo. Loo, jamani! Sio kurudi mahali fulani, na kusema, “Vema, kweli tulikuwa na Maji juzi, pale.” Tuna Maji leo, papa hapa, kwa maana Mwamba huo ulikuwa ni Kristo! Naye Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁰⁷ Mnaona, huo Mwamba uliwafuata Israeli. Kamwe wao hawakuufuata Mwamba huo, bali Mwamba huo uliwafuata. Amina. Israeli waliendelea na safari yao. Walikuwa na jambo moja tu la kufanya, hilo ni, kushika njia iliyo nyofu, moja kwa moja kuingia kwenye nchi ya ahadi. Nao Mwamba huo na maji hayo yakawafuata.

...ule Mwamba ukiwafuata:...

Wakorintho wa Kwanza hukwambia hivyo, mlango wa 10. Vema.

...Mwamba ule ulikuwa ni Kristo.

¹⁰⁸ Mungu alizichukua hukumu za watu na kuziweka juu ya Kristo, na kumpiga. Je! mliona, kulikuwako na ufa kwenye Mwamba huo, tangu hapo na kuendelea? Mwamba huo ulikuwa na ufa ndani yake, mahali ambapo Musa aliupiga. Naye Kristo alikuwa na ufa, wakati alipopigwa, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Kutoka kwenye huo Uzima yakaja Maji ya Uzima ambayo tunayafurahia sana leo!

¹⁰⁹ Sasa, kusudi uupokee huu Uzima, kumbuka, Uzima wa Kristo hukaa pamoja na Kanisa. Haleluya! Loo, laiti tungalitia nanga mawazo yetu hapo kwa dakika zingine kumi! Kristo haliachi Kanisa. “Nitakuwa pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Watu ndio humwacha Kristo, sio Kristo kuwaacha watu. Watu huliacha, kwa kutokuamini kwao. Wanamwacha Kristo, sio Kristo kuwaacha watu.

¹¹⁰ Israeli walikiacha kijito, si kijito kuwaacha Israeli. Mnaona? Kwa kuwa, Biblia inasema dhahiri ya kwamba, “Mwamba ule na maji yale yaliwafuata Israeli.” Yaliwafuata! Popote walipoenda, ulienda, pia.

¹¹¹ Loo, ningetaka, asubuhi ya leo, kama tungelikuwa na wakati, kufungua mlango wa kwanza wa Yohana, ambapo Yeye alisema, “Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga,

nimewapa ninyi. Popote uendapo, Bwana Mungu wako yu pamoja nawe. Usimwogope mtu yeyote. Uwe shujaa! Popote tu unapokanyaga, niko papo hapo pamoja nawe, hata iwe ni wapi.” Mungu akiambatana na YOSHUA!

¹¹² Mungu yeye yule anaambatana na Kanisa Lake asubuhi ya leo. Hebu na tuinywee Chemchemi hii huko ng’ambo. Popote utakapokanyaga, hapo ndipo Mungu atakapokuwa pamoja na wewe, kukutia maji na kukupa Uzima. “Nitakuwa pamoja nawe siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Kanuni za Mungu.

¹¹³ Sasa mnasema, “Basi, Ndugu Branham, ni kwa nini basi hatuyafanyi mambo tunayopaswa kuyafanya? Inakuwaje karama zetu na kadhalika kanisani hazinawiri, kufikia mahali zinapopaswa kuwa? Inakuwaje kanisa letu haliinuki kufikia mahali linapopaswa kuwa?” Watu, kwenye wakati wa majaribu, huanguka kama Israeli walivyofanya. Wanafikiri ya kwamba Mungu amewaacha.

¹¹⁴ Lakini, kumbukeni, Mwamba ule kamwe haukuwaacha Israeli. Israeli waliuacha ule Mwamba, walisahau kuhusu ule Mwamba kuwa pamoja nao wakati wote. Ulikuwa moja kwa moja pale, ulitembea moja kwa moja pamoja nao hadi mwisho wa safari. “Uliwafuata.” Haukuwa kwenye umbali usioweza kunenewa. Haukuwa kwenye umbali usioweza kusikika. Ama, haukuwa kwenye umbali usioweza kuonekana.

¹¹⁵ Wala na Kristo pia! Kwa Kanisa siku hizi, Yeye hayuko kwenye umbali asioweza kuzungumziwa. Baadhi yenu wamerudi nyuma, na kufanya lile lisilofaa, nanyi mmeipoteza ile furaha, nayo Maji yenu yamekauka. Yeye angali kwenye umbali anaoweza kuzungumziwa kutoka kwako. Yeye huambatana nawe. Anajua kila hatua unayochukua na kila kitu ufanyacho. Yeye ana hamu ya kukusikia ukimwita aje jukwaani.

¹¹⁶ Na huduma hii kubwa ya kipentekoste leo, Mungu anawangojea mumwite jukwaani. Hamko umbali asioweza kuzungumziwa nanyi. Ingawa tumekosea, na kutenda dhambi, na kumpa kisogo, na—na kufanya mambo tusiyoipaswa kufanya, lakini hata hivyo Yeye yuko pamoja nasi. Kristo alisema angekuwa pamoja nasi.

¹¹⁷ Biblia ilisema, “Maji hayo yaliwafuata wana wa Israeli.” Waliposhikwa na kiu, walijua maji hayo yalikuwa karibu.

¹¹⁸ Sasa, mambo haya yanadhibitiwa na kanuni. Mfumo wote wa Mungu umewekwa kwa kanuni. Sasa tutachukua... Hebu tusimame kwa dakika moja.

¹¹⁹ Hebu na tuuchukue ulimwengu. Unazunguka, kila saa ishirini na nne unafanya mzunguko mkamilifu, kamilifu kabisa. Huo, kamwe hatujaweza, pamoja na sayansi yetu yote, kuunda saa ya kudumisha majira kikamilifu. Kila baada ya kitambo kidogo, saa zilizo bora kuliko zote walizowahi kuunda, katika

mzunguko wa mwaka mmoja, zitaongeza ama kupoteza dakika nyingi. Bali ulimwengu haushindwi kamwe ila uko pale hasa kwenye sekunde. Ni mkamilifu sana hata wanasayansi leo, mamajusi wanaweza kukwambia, katika miaka ishirini tangu sasa ama miaka hamsini tangu sasa, vile hasa jua na mwezi zitakavyopishana. Wakati linapozunguka duara lake la saa ishirini na nne, na kugeuza wakati wake kuzunguka mzingo wake kwa majira, halikosei hata pigo moja. Haleluya! Ni kamilifu, kwa sababu linaenda kulingana na kanuni ya Mungu.

¹²⁰ Wanajua ni lini hasa hayo maji yatacupwa, kufikia barabara kwenye dakika, kwa kuwa wanajua ni wakati gani mwezi unaposhuka. Naye Mungu ameweka kila kitu kwenye utaratibu kwa kanuni fulani. Na wakati mwezi huo unaposhuka, maji yanakupwa pamoja nao. Mwezi huo unapotokeza, maji hapa yanajaa pamoja nao. Nao wanajua hakika, kwa kupima wakati, wakati mwezi huo utakaposhuka. Wanaweza kuiweka kwenye kalenda ya shajara kwa miaka kadhaa kabla, na kuwaambia, mpaka dakika, wakati maji hayo yatakapoanza kupwa. Hakika, kwa kuwa hivyo ndivyo mwezi unavyoondoka, kwa sababu umewekwa katika utaratibu wa kanuni za Mungu.

¹²¹ Nilikuwa nimesimama, hivi majuzi, karibu na Ziwa Michigan. Ndipo nikaenda kwenye Ziwa Superior, nikienda zangu Canada, huo mtandao mkubwa mno wa maji. Nami nikasimama pale, na nikawaza, “Ni maili ngapi kuyavuka maji haya sambamba hapa!” Ndipo baada ya mimi kuvuka Mich-... ama Ziwa Superior, ningeingia ndani ya Michigan, karibu mtandao sawa na huo wa maji. Na kufikia hapo, kutoka kwenye Ziwa Superior hadi Ziwa Michigan, kutoka Ziwa Michigan hadi Ziwa Ontario, na ninii tu... na Huron, na hayo maziwa yote pamoja. Ni mabilioni mangapi mara mabilioni mara mabilioni, na matangi yasiyohesabika ya maji safi yaliyo kwenye ziwa hilo!

¹²² Na huko Nevada, na katika Arizona, New Mexico, California Mashariki, kuna mamilioni ya ekari za mashamba yaliyokauka, yanayungua. Ambayo yana rutuba sana kiasi kwamba, kama maji hayo yangeweza kufika kwenye ardhi hiyo, taifa hili lingeweza kuulisha ulimwengu, pasiwepo watu wowote wenye njaa, na wawe na mabaki ya kutupa baharini. Hiyo ni kweli! Mamilioni ya ekari ambazo zingekuza tani mara mamilioni ya tani za viazi na kabichi, na maharagwe na—na saladi, na figili na seleri, na matango, na kadhalika. Ardhi hiyo ingezikuza, ina—inatamani tu ipate maji.

¹²³ Na haya hapa maji *hapa* juu, na huu hapa *udongo* hapa chini. Sasa tunaweza kuyaona, na tunajua yangejanya hivyo, kwa kuwa tunaweza kuyafanyia maji hayo uchunguzi na kuona ni safi, na kuufanyia udongo uchunguzi na kuona una rutuba. Sasa, shauku yote tunayoweza kuwa nayo, kamwe haitayaleta pamoja. Lakini, kuna kanuni, na kanuni hiyo ni kanuni ya uvutano. Sasa, kama tukifuata kanuni ya uvutano, tungeweza

kunyunyizia kila sehemu ya ardhi hiyo, tukiyatoa maji kwenye maziwa hayo na kuinyunyizia. Lakini itatubidi kufanya kazi kulingana na kanuni ya uvutano. Hatuwezi kuwa na shauku hata yakatoka kule. Hatuwezi kuyapigia yowe hata yakatoka kule. Hatuwezi kuyapigia kelele hata yakatoka kule. Inatubidi kufanya kazi kulingana na kanuni za uvutano, kuyapeleka kule. Mungu huweka kila kitu katika kanuni.

¹²⁴ Hapa, nilikuwa nikiwazia, sijui kama nilipata kuwaambia jambo hili, au la. Niliikuwa huko chini Kentucky, nikiwinda kuchakuro, pamoja na Ndugu Wood, yapata mwaka mmoja uliopita. Nasi... Kuchakuro kwa namna fulani walikuwa ni adimu, na kwa hiyo tukaenda nyumbani kwa jamaa fulani, kutafuta habari za kuwinda. Mtu fulani alikuwa na shamba la ekari kadhaa, na kwenye shamba hili kulikuwako na msitu mkubwa. Lakini Ndugu Wood akaniambia, kwamba, "Mtu huyo ni kafiri. Yeye ni—yeye ni asiyeamini." Kwa hiyo alisema ya kwamba alimfahamu, kwa hiyo yeye... ama baba yake alimfahamu, angeenda kule amwombe kama tungepata ruhusa ya kwenda kuwinda.

¹²⁵ Tukaenda kwa gari hata nyumbani kwa mwungwana huyo. Naye pamoja na mtu mwingine, wote wakiwa kwenye umri wa miaka ya sabini, walikuwa wameketi chini ya mtofaa. Basi Bw. Wood akamwendea mtu huyu, na akamwambia, "Naweza kuwinda kidogo huku kwako?" Naye akasema, "Vema," akasema, "sawa." Akasema, "Wewe ni Wood yupi? Wewe ni mvulana wa Jim Wood?"

Akasema, "Ndiyo."

¹²⁶ Akasema, "Vema, mzee Jim alikuwa ni mtu mnyofu, na kadhalika." Akasema, "Unaweza kuwinda popote utakapo, shambani mwangu. Nina ekari mia kadhaa hapa, jitudumie. Shuka uende mabondeni, popote utakapo. Jisikie tu nyumbani."

¹²⁷ Niliketi kwenye gari, kwa kuwa nilidhani mhubiri na kafiri hawataendana vizuri pamoja, kama tulikuwa tunaenda kuomba fadhili za kafiri.

¹²⁸ Kwa hiyo basi baada ya kitambo kidogo, Ndugu Wood akasema, "Vema, sasa, naweza kwenda pamoja na mchungaji wangu? Nafikiri ingekuwa ni sawa kwake kuja."

¹²⁹ Ndipo mzee huyu akageuka kwa fimbo yake, na akasema, "Wood, unataka kuniambia ya kwamba umejishusha sana, hata inakubidi kuwa na mhubiri kokote uendako?"

¹³⁰ Na kwa hiyo, nikawazia, baada ya hayo, ni afadhali nitoke kwenye gari. Kwa hiyo nikatoka kwenye gari, na nikazungumza na mzee huyo mwungwana kwa dakika chache. Naye akanijulisha upesi sana ya kwamba hakuwa na haja sana na wahubiri, kwa sababu alidhani walikuwa wakizungumzia kitu ambacho hawakujua kitu juu yake.

¹³¹ Akasema, “Wanafokea tu kitu wasichojua lolote kukihusu. Vema,” akasema, “mtu anapozungumza nami, ninamtaka ajue analozungumzia.” Sasa, hiyo ni hekima nzuri. Hiyo ni hekima nzuri. Akasema, “Sasa, kama mtu akizungumza nami, sitaki azungumzie kitu fulani, kinginecho, cha kudhania ambacho hajui chochote kukihusu. Ninamtaka azungumzie jambo ambalo anajua anachozungumzia.” Vema, niliheshimu hilo. Niliheshimu hilo katika mzee huyu mwungwana.

¹³² Na kwa hiyo nikasema, “Vema, hakika, hiyo ni kila mtu na maoni yake.”

¹³³ Ndipo akasema, “Kulikuwako na mhubiri mmoja aliyekuja hapa kwenye nchi hii, miaka michache iliyopita, aliyekuwa na mkutano huko Acton.” Kisha akasema, “Huyu mhubiri, usiku mmoja, akiwa ni mgeni humu nchini, alimwambia ma—mama mmoja aliyekuwa ameketi kwenye wasikilizaji, ‘Una lesa mfukoni mwako. Nawe ni Bibi. *Nanii*. Nawe una dada aliyemgonjwa juu ya kilima hapa. Jina lake ni *Nanii*. Yuafa, kwa kansa ya tumboni.’ Kisha kasema, ‘Chukua lesa hii ukaiweke juu ya dada yako, na umwambie, “BWANA ASEMA HIVI, hatakuwa, bali ataishi.”’”

¹³⁴ Akasema, “Mwanamke yuyu huyu alikuwa ni rafiki yetu.” Kisha kasema, “Tulimchukua huyu mwanamke... Lesa hii huko juu; ama mtu huyu, kwa mtu huyu.” Kwanza alisema, “Huyu mwanamke, mimi pamoja na mke wangu tulikuwa huko juu asubuhi hiyo na tulikuwa tumechukua, tukamhudumia huyu mwanamke. Naye alikuwa hawezi kabisa! Madaktari walikuwa wamemkatia tamaa, muda mrefu uliopita. Alikuwa mnyonge sana hata ilitubidi tumbebe kwa shuka, kumwinua kumweka kwenye chombo cha kujisaidia kitandani mwake, kisha kumrudisha. Kumgeuza kwenye shuka, alikuwa ni dhaifu sana.” Akasema, “Usiku mmoja, huko, kulitokea kelele kana kwamba walikuwa na mtu aliyekufa.”

¹³⁵ Huyu alikuwa ni Ben huko, akiwa na lesa hiyo, akiipeleka pale. Ninaamini ilikuwa ni wewe, sivyo, Ben? [Ndugu Ben anasema, “Amina. Amina.”—Mh.] Ilikuwa ni Ndugu Ben kule, akiichukua lesa hiyo, maana alimpeleka mwanamke huyo pale.

¹³⁶ Kisha kasema, “Kesho yake asubuhi, alikuwa akila pai ya tofaa iliyokaangwa.” Ndipo kasema, “Yeye hafanyi tu kazi zake mwenyewe, bali hufanya kazi ya jirani yake. Alikuwa amepona kabisa!” Akasema, “Sasa mara nyingi nimeshangaa. Kama nikipata kumwona mhubiri huyo, yeye alijua alilokuwa akizungumzia,” kasema, “Ni—ningetaka kuzungumza naye.”

¹³⁷ Ndugu Wood akaniangalia, nami nikamwangalia. Nimesimama pale, mchafu, na nimejaa jasho na ni mchafu, tulikuwa tumepiga kambi msituni, na—na damu ya kuchakuro imetutapakaa kote. Na kwa hiyo nikasema, “Vema,” nikasema,

“ni... Unamaanisha kwamba ungezungumza na jamaa huyu naye angekwambia jinsi ambavyo alifanya jambo hilo?”

Akasema, “Naam, bwana, hivyo ndivyo ninavyomaanisha.”

Nikasema, “Vema, hilo ni—hilo ni jambo jema.”

¹³⁸ Nilikuwa nikila moja ya matofaa yake. Maskini nyigu wadogo walikuwa wakiyavamia, mwajua, kwenye msimu wa mwaka wa majani kupukutika, Agosti. Kwa hiyo nilikuwa na tofaa hili dogo, nami nilikuwa nimeliiuma kidogo. Ndipo nikasema, “Hilo ni tofaa tamu sana.” Nikasema, “Huo mti umekuwa hapo kwa muda gani?”

¹³⁹ “Loo,” akasema, “niliupanda mti huo hapo, miaka thelathini ama arobaini iliyopita, ama kitu kama hicho.”

¹⁴⁰ “Naam, bwana.” Nikasema, “ningetaka tu kukuuliza swali.” Nikasema, “Vipi kamwe... Ninaona hayo matofaa yameanguka kutoka kwenye huo mti, na majani yake yanapukutika, na hapa ni katikati tu ya Agosti.” Kisha nikasema, “Hatujawa hata na kipindi cha baridi, wala hata hatujawa na barafu wala chochote kile, na hata hivyo majani yanapukutika kutoka kwenye huo mti. Mbona hivyo?”

Akasema, “Utomvu umeondoka mtini.”

“Loo,” nikasema, “kwani ulienda wapi?”

Akasema, “Chini kwenye mizizi.”

Nami nikasema, “Basi utakaa muda gani huko chini?”

Akasema, “Mpaka majira ya kuchipua.”

¹⁴¹ Nami nikasema, “Basi utapanda juu tena, na kuwaletaa majani mapya kwa ajili ya kivuli, matofaa mapya ya kula.”

Akasema, “Hiyo ni kweli. Kweli kabisa.”

¹⁴² Nikasema, “Vema, ninataka kukuuliza jambo fulani, bwana. Unazungumza juu ya jamaa hawa ambao hawajui wanalozungumzia.” Nikasema, “Je! ungeweza kunielezea ni Akili gani inayoufanya huo utomvu kuondoka kwenye mti huo? Kama ungalikaa mle kote katika majira ya baridi kali, huo mti ungekufa. Ungeuua mti huo. Chembe ya uhai iko kwenye utomvu huo.” Kwa hiyo nikasema, “Ungeuua mti huo. Ni Akili gani inayoufanya huo utomvu kuondoka kwenye huo mti, ukaingia mizizini, na kukaa mpaka kwenye majira ya kuchipua, na kisha upande juu tena na kuzaa matofaa zaidi?” Nikasema, “Tia maji kwenye ndoo na uiweke kwenye mlingoti, na uone kama, kwenye Agosti, yatateremka chini ya huo mlingoti na kurudi kwenye majira ya kuchipua. Unaona?” Nikasema, “Kuna kanuni fulani, kuna kanuni ya maumbile. Akili fulani iliweka kanuni hii katika utaratibu. Si hivyo tu, bali Akili hiyo hiyo haina budi kutekeleza hizo kanuni, ambazo huusukuma chini kwenye mizizi ya mti huo, kisha ukarudi.”

Akasema, “Kamwe sikuwa nimeliwazia hilo.”

¹⁴³ Nikasema, “Je! waweza...Kama ungaliweza kujua Akili hiyo inayoufanya huo utomvu kutoka kwenye matawi ya huo mti, ukaingia kwenye mizizi na kurudi, hiyo ndiyo Akili ile ile iliyoniambia huko usiku ule, ‘Nenda, ukaiweke leso hiyo juu ya mwanamke huyo.’”

Akasema, “Na wewe ndiwe yule mhubiri?”

Nikasema, “Naam, bwana, hiyo ni kweli.”

¹⁴⁴ Mwaka uliopita nilikuwa huko (yeye ameshaondoka), na mjane wake alipokuwa ameketi barazani, akimenya matofaa, kutoka kwenye mti uo huo. Ndugu...Kwanza walikuwa watufukuze, hawakujua tulikuwa ni akina nani. Nami nikaenda na kumwambia kuhusu hilo, ya kwamba tulikuwa na ruhusa ya kutoka kwa mumewe. Na nikamwambia hivyo, kasema, “Yeye alimkiri Kristo kikamilifu kabla hajafa.”

¹⁴⁵ Mnaona, ni kitu gani kinachoufanya huo mti, ni Akili gani inayousukuma huo chini? Ni kanuni. Ni kanuni ambayo Mungu ameiweka katika utaratibu. Na kanuni hiyo ni kanuni ya Mungu ambayo italishughulikia jambo husika. Amina.

¹⁴⁶ Mwajua, sijali jinsi unavyolia, na kusema—kusema sasa, “Halitaninii, jua halitaangaza tena msimu huu wa kiangazi.” Litaangaza, kwa vyovyote. Ni kiasi gani utasema, “Si—si—sitauruhusu usiku uje.” Utakuja, kwa vyovyote. Kwa sababu kitu hiki tunachoishi juu yake, kinachoitwa ulimwengu, kimedhibitiwa na kanuni ya Mungu.

¹⁴⁷ Sasa, ndugu na dada, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Basi, kama tumezaliwa mara ya pili na Roho wa Mungu! Mungu hana sehemu ndogo dhaifu na sehemu kubwa zenye nguvu, Yeye kwa jumla ni Mungu! Na kama ulikuwa na kiasi cha Mungu cha kutosha ndani yako, mpaka ilikuwa angalau tu ni kivuli, hizo ni nguvu za kutosha kuumba dunia mpya. Hizo ni nguvu za kutosha kufanya mwezi mpya na mfumo mpya. Ni Mungu, na ina nguvu! Na sasa hivi kila mwaminio hapa ndani yuna Uzima wa Milele, ambao ni, Roho wa Mungu ndani yako; Nguvu za kutosha zitakazowafufua wafu, zitakazowaponya wagonjwa, zitakazoiweka mizingo katika hali nzuri. Lakini wewe, anaongozwa na kanuni fulani, Roho huyo aliye ndani yako. Ninyi ni wana na binti za Mungu. Roho yeye yule uliye Naye ndani yako, utajifufua mwenyewe katika siku ya ufufuo.

¹⁴⁸ Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, wakati alipokufa, nafsi Yake ilishuka Kuzimuni, “Na akawahubiri roho waliokuwa kifungoni, nafsi zilizokuwa kifungoni, ambao hawakutubu katika uvumilivu wa siku za Nuhu.” Mwili wake ukaingia kaburini. Lakini kabla hajafa, Yeye aliikabidhi Roho Yake mikononi mwa Mungu. Roho Yake ikaenda kwa Mungu; nafsi Yake ikaenda Kuzimuni; nao mwili Wake ukaenda kaburini. Naye Yesu alizuiliwa asifufuke mpaka Maandiko yaweze kutimia. Asingeweza kurudi, kwa sababu ilimbidi

kukaa kaburini siku tatu usiku na mchana. Lakini wakati Maandiko yote yalipotimizwa, kizuizi hiki kiliondolewa; Roho Yake ikashuka kwenye nafsi Yake, nafsi Yake kwenye mwili Wake, Naye akafufuka tena.

¹⁴⁹ Nasi tunapokufa, nafsi zetu zitaenda chini ya madhabahu ya Mungu; ambapo nilipewa majaliwa ya kupaona, asubuhi chache zilizopita, kama mjuavyo, katika ono, ambapo Biblia inazungumza habari zake. “Roho zetu zitaenda kwa Mungu aliyezitoa, na miili yetu itarudi kwenye mavumbi ya ardhi.” Lakini siku moja, wakati Maandiko yatakapotimizwa, roho zetu zitaachiliwa kutoka kwa Mungu, zitaichukua nafsi, nayo nafsi iuende mwili. Nazo Nguvu zitakazotufua, ziko moja kwa moja ndani yetu sasa! Sasa tuko katika ulimwengu wa Roho. Sasa tuko katika Nguvu za ufufuo.

¹⁵⁰ Kama kusingekuwako na kanuni zake, wana na binti za Mungu wangelijumbia ulimwengu hapa na waende wakaishi maisha ya peke yao kwenye huo. Una Nguvu za kufanya hivyo ndani yako. Kama una kivuli cha Nguvu za Mungu ndani yako, una Nguvu za kufanya hivyo. Mungu ni muweza wa yote. Mnaona ninalomaanisha? Nguvu zilizomo ndani yako zitaufanya. Ungeweza kuunena ulimwengu ukaweko na uende ukaishi humo. Haleluya! Haya basi.

¹⁵¹ Hizo ndizo Nguvu zilizomo Kanisani sasa, bali zinadhibitiwa na kanuni fulani. Na hiyo kanuni si “kushika lundo la amri.” Ni kanuni ya imani. Yesu alisema, “Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.” Na kama unaweza kuliadini, chochote kile Mungu ataiongoza nafsi yako kuamini, hicho ni chako. Kila mahali nyayo za miguu yako zinapoweza kukanyaga, kwa imani, Mungu anakupa wewe. Amina! Ni pako, unapamiliki, ikiwa unaweza kupata ufunguo wa hii kanuni ya imani inayokufungulia huo. Unaona ninalomaanisha? Nguvu hizo zinadhibitiwa na... Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, wewe ni binti ya Mungu, hizo hazikuachi. Ziko pamoja nawe wakati wote. Lakini, imani yako huziacha, bali zingalipo. Haleluya!

¹⁵² Wakati unapookolewa, Mungu hukupa imani kuinuka kutoka kwenye kinyaa cha dunia. Imani yako inashinda mambo ya ulimwengu. Imani yako ni nini? Imani yako katika tendo hilo ambalo Mungu amelitenda ndani yako, kukufanya mwana wa Mungu. Unaachana na kusema uongo kwako, unaachana na kuiba kwako, unaachana na kunywa pombe kwako, kwa kuwa imani yako inakuinua juu yake. Amina. Kama hufanyi hivyo, huna imani yoyote. “Na kwa imani unaokolewa, na hiyo ni kwa neema.”

¹⁵³ Kadiri ya imani yako itakayoachiliwa, hicho ndicho kiasi cha Nguvu unazoweza kuwa nazo, kwa kuwa ndani yako mnaishi Nguvu za kufanya Mbingu na nchi. Mungu anaishi ndani yako, nanyi ni wana na binti za Mungu. Amina! Haya basi. Lakini,

ni imani yako. Yesu alisema, “Kulingana na imani yako, na iwe kwako. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usitilie shaka, bali uamini yale umesema.”

¹⁵⁴ Basi tunapaswa kuwa watu, wa namna gani, tukiwa na imani katika huyu Kristo mkuu anayekomboa anayeishi ndani yetu, Mwamba huu uliopigwa ambao hauliachi Kanisa? “Niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari,” Uwepo udumuo daima wa Kisima hiki kikuu kinachobubujika cha wokovu na Nguvu zilizomiminwa kutoka Kalvari hadi Kanisani, Uwepo udumuo daima wa Mungu aliye hai, Mwamba mkuu uliopigwa, unaobubujika na kuambatana nasi katika safari yetu.

¹⁵⁵ Israeli ilipoteza imani yake. Waliondoka njiani. Walianza kutamani sufuria za nyama. Kama wangelidumu na imani, na wakiamini ya kwamba Mungu alikuwa anaenda kuwapeleka kwenye nchi ile, kusingekuwako na chochote kingaliwazuia. Walikuwa tayari wamezifungua bahari, walikuwa wameleta mapigo juu ya adui zao, walikuwa wamewasulibisha adui zao nyuma yao, na walikuwa wameenda wakaingia kwenye nchi ile, na bado wasingekuwako na imani ya kutosha kuingia kwenye ahadi ile.

¹⁵⁶ Yoshua na Kalebu walikuwa na hiyo imani! Walisema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kushinda chochote ambacho kingekuja mbele zetu.”

¹⁵⁷ Hiyo ndiyo shida ya kanisa. Tunaweza kushinda kila ugonjwa. Tuna Nguvu ndani yetu. Sisi ni wana na binti za Mungu, hakuna kitu kinachoweza kusimama mbele zetu. Jambo la pekee, Yeye anataka kumpata mtu fulani atakayeliadini, ambaye ataamini kile Mungu amewafanyia tayari. Sio *tutakuwa*; tuko sasa! Nao Uwepo unaoishi daima wa Roho uko pamoja nasi. Amina! Haya basi.

¹⁵⁸ Hilo ndilo nililomaanisha wakati nilipozungumzia somo hilo asubuhi ya leo, *Maji Yaliyopo Daima Yatokayo Mwambani*. Maji yaliyopo daima yatokayo Mwambani yapo hapa sasa, hayo Maji yaliyopo daima yatokayo kwenye Mwamba uliopigwa pale Kalvari. Wakati huyo Roho Mtakatifu alipotoka ndani Yake pale Kalvari, huyo aliyerejea juu ya Kanisa kwenye Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu yuyo huyo yupo asubuhi ya leo. Naye ametupa ahadi!

¹⁵⁹ Hiyo ndiyo sababu, nilipotembea mbele ya wagonjwa, wakati Yeye aliponiagiza huko ng’ambo, ninaliamini; Mungu alisema hivyo! Hivyo ndivyo maono hutukia; Mungu aliliahidi! Mungu hawezi kusema uongo.

¹⁶⁰ Aminini! Huna budi kuamini hilo. Hapana budi pawe na kitu pale, fungua valvu hiyo, fungua kitu hicho kikuwezeshe kuingia ndani yake. Tunachohitaji leo hii si kuomba tupate Nguvu nyingi zaidi. Una Nguvu za kutosha kuumba dunia mpya.

Unachohitaji ni imani ya kuzitumia Nguvu hizo. Unachohitaji ni kuyadhibiti hayo maisha, na kuishi maisha ya kitauwa sana, hata unapomwomba Mungu chochote, unajua! Tuna imani na Mungu, juu ya hilo. Tunajua, kama tukitii amri Zake, Yeye hatatunyima kitu chochote chema, kama tukitembea na Yeye. Mungu akitembea pamoja nasi. Loo, jamani!

¹⁶¹ Walikuwa na jambo moja tu la kufanya. Walikuwa na jambo moja tu la kufanya, hilo ni, kudumu moja kwa moja safarini. Si kutangatanga *huku*, na kutangatanga *huko*; bali kudumu safarini! Kanisa lina jambo moja tu la kufanya, kudumu safarini! Walikuwa na Nguzo ya Moto, waliyokuwa nayo, ya kujidumisha safarini kwa kuifuata hiyo Nguzo ya Moto. Hiyo ndiyo iliyowaongoza. Kitu chao wangaliweza kukiona, kilikuwa ni hiyo Nguzo ya Moto. Waliiona ikitenda kazi kupitia Musa, nao wakajua ya kwamba yeye alikuwa ndiye kiongozi.

¹⁶² Leo tuna Neno. Tunalifuata Neno. Na tunaliona Neno likifanya kazi katika waaminio, nasi tunajua ni kweli, basi. Mungu akitenda kazi pamoja nasi, akilithibitisha Neno kwa ishara zinazofuata! Tunadumu na Neno. Neno linazaa matokeo.

¹⁶³ Walidumu na Musa. Kwa sababu, Nguzo ya Moto, Musa aliifuata Hiyo. Nao wakafuata. Walipoanza kugeuka dhidi ya Musa, na kunung'unika dhidi ya Mungu na dhidi ya Musa, walianza kutangatanga upande mmoja na mwingine. Taabu zikaingia. Hakika.

¹⁶⁴ Tunadumu na Neno, na Neno linazaa ishara. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao wanaoliamini Neno." Mnaona, linakaa pamoja na... Ukidumu na Neno, Neno linazaa ishara. Lakini, Musa, yeye alifanya nini?

¹⁶⁵ Walitangatanga, nao wakafanya nini? Waliacha njia, ndipo wakapoteza ruzuku yao ya maji.

¹⁶⁶ Nafikiri hilo ndilo kanisa limefanya leo hii. Limeondoka kwenye njia ya Maandiko. Wameingia kwenye itikadi. Wamepotea kwenye mambo madogo wasiyopaswa kufanya. Walichukua mambo. Walichukua mambo kama Imani ya Mitume. Unaipata wapi hiyo katika Biblia? Walichukua katekismo wanzosoma. Walichukua madhehebu badala ya tukio. Walichukua kupeana mikono badala ya tukio la kuzaliwa mara ya pili. Walichukua kunyunyizia badala ya ubatizo wa maji. Walichukua taratibu oву, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," wakati hakuna kitu kama hicho katika Biblia. Biblia ilisema, "Katika Jina la Yesu Kristo!" Kuna jambo moja tu la kufanya kama ukitaka Maji yale yale, rudi njiani tena. Rudi kwenye... Yeye hajaondoka; Yeye angali hapa. Mnachukua kanuni za imani badala ya Kristo. Mnapotelea kwenye hamaki.

¹⁶⁷ Mtu alisema, "Vema, mimi ni Mmethodisti." Huyu mwingine anasema, "Mimi ni Mbaptisti." Hiyo inaonyesha wewe si Mkristo, basi. Sisi ni wa Kristo! Sisi ni mali Yake. Unasema,

“Vema, kama mimi, Mbaptisti.” Kama hivyo tu ndivyo ulivyo, basi wewe si wa Kristo, wewe ni Mbaptisti. Ukisema, “Vema, mimi ni Mpentekoste.” Kama wewe ni mpentekoste tu kwa dhehebu, hivyo tu ndivyo ulivyo wewe.

¹⁶⁸ Lakini, kama una tukio la kipentekoste! Nalo Neno la kipentekoste litazaa tukio la kipentekoste! Fuata jambo lile lile wale wanafunzi walilofuata, kaa pale juu mpaka umejazwa na Roho Mtakatifu.

¹⁶⁹ Halafu basi iwapo utaenda kinyume na Neno, hiyo roho iliyo ndani yako inaenda kinyume na yale Neno lisemayo, basi si Roho Mtakatifu. Ni ibilisi akimwiga Roho Mtakatifu. Unaona mahali tulipofikia nalo? Loo, baadhi yetu walinena kwa lugha, tulikuwa na vipindi vya kupiga makelele na kadhalika namna hiyo, na kukana mambo haya mengine yote. Tuliruhusu kila kitu ambacho hakikuwako katika Maandiko kiingie kanisani. Tumefika wapi siku hizi? Tumerudi kwenye jangwa lingine, dhehebu lililokauka kabisa. Tuliunda madhehebu, na tukapoteza Maji yetu. Hivyo ndivyo Pentekoste ilivyofanya hasa. Wakati ilipoanza kujiundia madhehebu, ilianza kuvunja ushirika, na kusema, “Vema, sasa hatutashirikiana, kama jamaa huyu anaamini *hilo*.”

¹⁷⁰ Endeleeni, dumuni pamoja naye mpaka atakapofikia Neno la Kweli, ujuzi wa Kweli. Chochote kile, kiacheni, hata hivyo. Endeleni tu, iweni kama ndugu.

¹⁷¹ Lakini, loo, ilitubidi kujiundia dhehebu, na kusema, “Vema, kwa kuwa wewe si wa Umoja, kwa kuwa wewe si wa Uwili, ama wa Utatu, ama namna *hii*, hatutakuwa na ushirika na wewe.” Ndipo tunapofanya jambo hilo, tunafanya nini? Tunajirudisha moja kwa moja kwenye jangwa tena. Hiyo ni kweli!

¹⁷² Lakini, kumbukeni, wakati Israeli walipoiacha njia, njia ya kwenda kwenye nchi ya ahadi, Mwamba haukuwaacha; Ulikaa pale pale, vivyo hivyo na maji pia. Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu, anakaa pale pale. Haitubidi kurudi nyuma.

¹⁷³ Sasa, hapa Mungu anatufundisha jambo kubwa. Mungu anatufundisha hapa somo fulani. Kristo alipigwa mara moja, akitupa tukio la kipentekoste, mara moja, kwa ajili ya wote. Sasa, wakati Mwamba huo ulipopigwa, haukupaswa kupigwa tena. Ulipigwa mara moja tu.

¹⁷⁴ Musa alifanya kosa kwa kuupiga mara ya pili, ikionyesha udhaifu wa imani yake katika Upatanisho. Lakini hapo Kristo alipopigwa mara moja, tunajua haitambidi kupigwa tena. Vema, Musa alikuwa akifanya nini? Musa alikuwa akianzisha jambo jipya, akijaribu kuunda kitu kipya.

¹⁷⁵ Na hivyo ndivyo makasisi wetu wamefanya leo. Wamejaribu kuunda kitu kipya. “Tutajiundia Assemblies of God. Tutajiundia Pentecostal Church of God. Tutajiundia Halmashauri Kuu.

Tutajiundia *hili, lile*, ama *linginelo*.” Hivyo sivyo vile Mungu alivyofanya. Hilo halikuwa ni wazo Lake.

¹⁷⁶ Kristo alipigwa mara moja. Hilo ndilo tukio la asili. Hiyo ndiyo njia ya asili. Kwenye Siku ya Pentekoste, Petro alisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo.”

¹⁷⁷ “Tunanyunyizia katika jina la ‘Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,’ kutoa kila namna ya kanuni za imani na kadhalika kuhusu Hilo.” Tunapoondoka kwenye Neno, si ajabu hatuwezi kufikia mahali popote. Mnaona?

¹⁷⁸ Mungu hutufundisha somo. Musa hakupaswa kusema, “Sasa tutaanzisha kitu fulani kipya hapa sasa, nasi tutajiundia dhehebu na tutaunda kanisa Katoliki.” Hilo ndilo jambo la kwanza walilofanya. La, ndipo baada ya kitambo kidogo, “Vema, tutaanzisha kitu fulani kipya kutokana na hilo, tutajiundia la Kilutheri.” Ndipo likaja la Kianglikana, na halafu la Kibaptisti, na kadhalika, na la Kikampbeli, na Church of Christ, na mpinga Kristo, na vitu vingine vyote. Mnaona, wote walianza kwenda, mmoja baada ya mwingine, mmoja baada ya mwingine, wakijiundia madhehebu na mashirika. Hilo lilikuwa silo. Mnaona hapo kile wanachofanya? Wanaupiga Mwamba tena, kuanzisha kitu kipya. Hatuhitaji fundisho jipya.

¹⁷⁹ Kila mtu katika Biblia alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Kila mtu katika Biblia aliyempata Roho Mtakatifu, alipitia kwenye njia ya Mungu, jinsi hasa Mungu alivyoiweka. Walifanya jambo lile lile. Walikuwa na tukio lile lile. Ishara zile zile zilifuatana nao. Kazi zile zile ziliwafuata. Kwa nini? Waliishi kwa ule Mwamba. Walipata Maji yale yale.

¹⁸⁰ Na, leo, sababu ya sisi kuwa na kanuni nyingi sana za imani na madhehebu, ni kwa sababu tunaanzisha kitu kipya. Hatuhitaji kitu chochote kipya. Rudini!

¹⁸¹ Musa hakupaswa kuupiga Mwamba huo tena, kuanzisha kitu kipya. Alipaswa kuwanenea, kuhusu Mwamba wa asili. Loo, ninatumaini mnalipata hilo! Musa alipaswa kunena kuhusu ule Mwamba wa asili, uliopigwa; si kujaribu kuupiga tena, sio kujaribu kuanzisha kitu kipya, bali kunena na Kitu hicho cha zamani!

¹⁸² Mungu, nisaidie! Kama nikifa ombaomba, mimbarani, nitanena juu ya Mwamba wa asili! Nitanena juu ya tukio la asili. Nitanena juu ya Maandiko ya asili yaliyowapa ubatizo wa Roho Mtakatifu, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Uwepo uliopo daima wa Maji yanayobubujika kutoka kwenye Mwamba ungali pamoja nasi. Utaleta jambo lile lile. Utaleta maono. Utaleta uponyaji. Utaleta unabii. Utaleta kila kitu walichofanya.

183 Wakati Israeli waliponyoshwa katika Maandiko tena, na wakarudi njiani, walienda mpaka kwenye nchi ya ahadi. Ila iliwachukua muda wa miaka arobaini.

184 Pentekoste imekuwa karibu miaka arobaini ama hamsini, wakizurura kote jangwani. Rudini kwenye Mwamba! Unaonekana. Huu hapa, umeandikwa papa hapa kwenye Neno. Roho Mtakatifu yupo hapa akifanya jambo lile lile alilofanya daima, kwa hiyo Uwepo uliopo daima wa Maji upo hapa. Rudini tu Kwake, rudini kwa yaliyotangulia, ya asili. Ilikuwa je katika ya asili?

185 “Vema, walipeana mikono na mhubiri”? Hakuna kitu kama hicho. “Walibatizwa katika jina la ‘Baba, Mwana, Roho Mtakatifu’”? Hakuna kitu kama hicho. Hakuna watu katika Biblia, mahali popote, ama (nje ya muda wa miaka mia tatu) nje ya Biblia, aliyebatizwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Hizo ni kanuni za imani ya Katoliki, si fundisho la Biblia. Mnaona?

186 Walikuwa na Roho Mtakatifu. Ishara hizi zilifuatana na hao walioamini. Zitafanya jambo hilo tena leo. Mwamba huo ungali unaishi daima kama ulivyowahi kuwa, Mwamba huo uliopigwa!

187 Hebu tusiseme, “Vema, sasa wewe njoo huku ukajiunge na kanisa letu la Kipentekoste, uingie kwenye milki zetu za Kipentekoste.” “La, wewe njoo huku ukajiunge na la Kibaptisti, ama la Kimethodisti, ama la Kipresbiteri, ama la Katoliki.” Hicho ni kitu gani? Huko ni kuupiga Mwamba mara nyingine tena, kujaribu kuanzisha kitu kipya.

188 Waambie, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo,” kwa ondoleo la dhambi zao, “na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa mmerudi njiani, mmerudi kwenye Maji yale yale. Maji yayo hayo yatatoa burudisho lile lile. Yataupa mwili kusuguliwa kule kule. Yatatoa nguvu zile zile za kuosha. Yatatoa nguvu zile zile za uponyaji. Yatafanya jambo lile lile yaliyofanya wakati ule, kama tutarudi tu kwenye Roho yeye yule.

189 Uhai uliomo kwenye mzabibu utazaa mizabibu. Kama ulizaa mwaka jana, utazaa kitu kile kile mwaka huu. Hiyo ni kanuni ya Mungu. Kanuni ya Mungu ni kwamba, kama huu ni mzabibu, achana nao, utazaa mizabibu. Unaweza kuuzalisha na kitu kingine, bali hata hivyo achana nao nao utarudi kwenye mizabibu ile ile tena.

190 Kwa hiyo tumelizalisha kanisa na Upentekoste, na Ubaptisti, na Umethodisti, na Upresbiteri, na—na Uanglikana, na kila namna nyingine ya itikadi. Kwa nini msiliache peke yake? Rudini kwenye Mzabibu, utarudi kwenye Nguvu zile zile. Amina! Amina! Ninapenda hilo.

191 “Anzisha kitu kipya.” Jambo lile lile ambalo tumelifanya. Si...kujaribu kuonyesha mamlaka yetu. “Daktari *Nanii* ndiye

mwanzilishi wa kanisa *Fulani-fulani* la *ninii*.” Kwa hiyo, hilo lilikuwa silo.

¹⁹² Hivyo ndivyo Musa alivyosema, “Nitawaonyesha kile ninachoweza kufanya. Nitayaleta, hata hivyo!” Akaupiga, hayakutokea. Akapiga makelele tena, “Nitaonyesha kile ninachoweza kufanya!” Mungu alikuwa na neno naye kwa ajili ya jambo hilo.

¹⁹³ Msifikiri, kama wewe “ukishikilia tu kwenye dhehebu fulani.” Mungu atakuwa na neno nawe kwa jambo hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Hamna budi kurudi kwenye ile ya asili. Rudini.

¹⁹⁴ Hebu zungumza tu na watu. (Usiwaambie, “Ninyi njoni mkajiunge na kanisa letu. Njoni mkaikariri kanuni yetu ya imani.”) “Rudini mkatubu, na mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu; nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kama moyo wako uko sahihi. Nazo ishara hizi zitawafuata waaminio. Kundi la waaminio, ishara hizi zitafuatana nao.” Kwa sababu gani? Mwamba, Mwamba uliopigwa na Maji Yake ya Uzima yanatoka moja kwa moja, yakitoa kitu kile kile Yeye alichokitoa kule nyuma. Hayawezi kujizuia. Loo, naam.

¹⁹⁵ Tunataka kujigamba, na kusema, “Sisi ni Methodisti, na Baptisti.”

¹⁹⁶ Sema tu na Mwamba, Yeye Yupo daima. Usijaribu kujiunga Nao. Nilikuwa “nimejiunga” hapa chini. Usijaribu kujiunga Nao. Huwezi kujiunga na Huu, hilo ni jambo la hakika. Unaweza kujiunga na Methodist, unaweza kujiunga na Baptisti, unaweza kujiunga na Wapentekoste, unaweza kujiunga na Waanglikana, lakini huwezi kujiunga na Huu. La. Huna budi kujazwa na Huyu. Usijiunge Nao; jazwa tu Naye. Hivyo tu. Ni kujazwa na nini? Kujazwa na Nguvu, kujazwa na Roho, kujazwa na Uzima, kujazwa na furaha, amani, uvumilivu, upole, wema, Nguvu za Roho Mtakatifu maishani mwako, kwa kuwa Uwepo wa milele umo mle. Kumbukeni.

Itanibidi kufunga, maana inachelewa.

¹⁹⁷ Lakini, kumbukeni, huo Mwamba kamwe haukuwaacha. Kamwe haukuwaacha. Naye Kristo kamwe hatatuacha; Kristo alisema, “Nitakuwa pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari.” Hiyo ni kweli? Nao huo Mwamba ulikaa pamoja nao kote kote kutoka Horebu hata Nebo. Ulikaa. Mpaka huko Yordani, ulikuwa ungali pale. Ee Mungu, ninataka kuuona huko Yordani!

¹⁹⁸ Musa, wakati alipokuwa huko Yordani, Mwamba ulikuwa pamoja naye kote njiani. Naye alikuwa amesimama pale juu, akiangalia chini kwenye ku—kundi la watu waliokuwa wamerudi nyuma na kumwacha Mungu. Moyo wake ulikuwa ukiwaonea shauku. Naye akaangalia ng’ambo ya Yordani. Huyu hapo kwenye Yordani. Yordani, kiroho, ndiyo ninayozungumzia.

Naye huyu hapa amesimama pale, mauti ilikuwa inamkaribia. Lakini akaangalia, na hapo karibu naye ulikuwako ule Mwamba. Yeye aliukanyaga tu huo Mwamba, nao Malaika wakaja, wakamchukua.

¹⁹⁹ “Sitakuacha kamwe wala sitakupungukia.” Haijalishi nyakati zinakuwa ni ngumu jinsi gani, jinsi gani tunazeeka, ni kifo cha aina gani tunachokufa, kumbukeni, Mwamba huo utakuwako pale Yordani. Hautatuacha kamwe wala kutupungukia. Kumbuka tu hilo. Uwepo udumuo wa Maji yatokayo Mwambani utakuwa pamoja nasi kote katika maisha, na hata kwenye Yordani.

²⁰⁰ Na tuinamishe vichwa vyetu. [Ndugu mmoja katika kusanyiko anatoa ujumbe katika unabii—Mh.]

²⁰¹ Wakati huyo Roho anapotembea miongoni mwetu, Roho wa Mungu akitembea miongoni mwetu, je! kungekuwako na wale hapa asubuhi ya leo wasiomjua Kristo, na wewe—wewe hujaukaribia huo Mwamba, hamko katika hali ya kuzungumza Nao asubuhi ya leo? Lakini unajua Upo. Uangalie ukitenda kazi kila mahali, mwone Yeye akizunguka kila mahali, uuone ukitembea juu ya watu. Huo ni Uwepo udumuo wa hayo Maji. Huo ni wokovu. Huyu Ndiye Roho anayevijaza vikombe vyao kufikia mahali ambapo wasingeweza kutulia tena, kitu fulani hakina budi kutokea. Wala humjui, ungetaka kuinua mkono wako na kusema, “Niombe, Ndugu Branham. Sasa ninataka kumjua. Na ninataka kuzungumza na Yeye, na ninataka kumjua kama utimilifu wa Roho Wake. Ninataka kujua ya kwamba Yeye yupo papa hapa kando yangu, wakati wote. Ninaamini yupo. Lakini ninataka kuwa katika hali ya kuzungumza. Nami nina kiu, na ninamwonea Mungu njaa. Ninataka kumjua vizuri zaidi?”

²⁰² Mungu akubariki, bwana. Na Mungu akubariki, bwana. Na wewe, ndugu. Wewe, naam, huko nyuma kabisa. Hapa chini, mama, naam. Naam, mama. Tunaiona mikono yenu, na Mungu anaiona. Mungu akubariki, ewe kijana mwanamume. Mungu akubariki. Na wewe, mama. Amina. Mungu akubariki. Ubarikiwe, dada. Mtu mwingine sasa, katika muda huu wa utulivu. Mungu akubariki, huko nyuma kabisa, jamaa mdogo.

²⁰³ Wazia hilo. Liwazie, Uwepo udumuo wa Maji yatokayo Mwambani, Roho yule yule; ambaye Yeye alipiga mayowe pale kwenye siku ya hukumu kwa ajili Yake, wakati alipoichukua hukumu yetu. Na fimbo ya hasira za Mungu ikampiga, nazo dhambi zako zilikuwa zimefungwa kwenye fimbo hiyo, nayo ikampiga, ndipo Damu Yake na maji yakabubujika kutoka Kwake. Akasema, “Baba, katika mikono Yako naiweka Roho Yangu.” Na kwenye Siku ya Pentekoste, akaja apate kuambatana nasi katika safari. Naye yuko karibu sana sasa.

204 Wakati ulipoanza kwenda, na ukazurura mbali na Nyumbani; sema, “Bwana, naja Nyumbani.” Wakati tukiimba huu, kama ungetaka kuja madhabahuni na kufanya uwekaji wakfu upya, pia, wa nafsi yako, kwa Kristo? Amina.

Nimezurura mbali na Mungu, (kutoka njiani)
 Sasa naja nyumbani;
 Njia ya kutokuamini (ni dhambi) nimeipitia
 kwa muda mrefu sana,
 Bwana, naja nyumbani.
 Naja nyumbani, naja nyumbani,
 Kamwe sitazurura tena;
 Ifungue kabisa mikono Yako ya upendo,
 Sasa, Bwana, naja nyumbani.

205 [Ndugu Branham anaendelea kuuvumisha, *Bwana, Naja Nyumbani*—Mh.]

206 Wavulana watatu wadogo ndio kwanza wajitokeze, upesi sana, machozi machoni mwao, wanapiga magoti kando ya madhabahu. Hakika, wamesamehewa. Walisamehewa hata kabla hawajaondoka vitini mwao, hapo maskini mioyo yao ilipofanya uamuzi. Walikuja tu mbele na kupiga magoti hapa, kuwafanya watu wajue hilo, kwamba wako upande wa nani, asubuhi hii.

207 Ningefikiri ya kwamba kungekuwako na watu wenye umri mkubwa zaidi wangetaka kufanya hivi, wangetaka tu kupiga magoti, na kusema, “Bwana, ni—nimezurura mbali na njia. Nimekuwa na mashaka mengi sana, na wakati mwingine nilizurura na kuingia dhambini. Sasa na—nataka kurudi kabla haijachelewa sana. Mungu, ni—ningetaka kuja. Ningetaka tu kuja na kupiga magoti.” Amina.

208 Sasa, wasichana watatu wadogo wa Arthur Beam, karibu wamelingana kwa kimo, walipanda huku, wakapiga magoti.

209 Anayekuja mbele ni msichana mdogo ambaye ndiyo tu amempata ndugu mdogo mpya nyumbani. Hivi majuzi nilikuwa tu nimeketi; Bibi Wood akaja na kuniambia, akasema huyu dada alikuwa akienda hospitalini kujifungua mtoto. Roho Mtakatifu akasema, “Nenda ukawaambie atakuwa ni mvulana.” Wakati alipozaliwa, alikuwa ni mvulana mdogo.

210 Inaonekana ni watoto asubuhi ya leo, jamaa hawa wadogo wanaotoka kwenye darasa dogo la Dada Arnold, wakiyaweka maisha yao wakfu. Madhabahu yote, kwenye mkono wangu wa kulia, yamejaa watoto wadogo. Linge kuwa ni jambo jema kama tungeimba wimbo, madhabahu, kwa watu wengine, (sivyo?) watu wazima.

Sasa, Bwana, naja nyumbani.

211 [Ndugu Branham anazungumza na watoto madhabahuni, wakati akiimba hapa na pale, *Bwana, Naja Nyumbani*—Mh.]

Naja nyumbani, naja nyumbani,
 Kamwe sitazurura tena;
 Ifungue kabisa mikono Yako ya upendo,
 Bwana, naja nyumbani.

Nimechoshwa na dhambi na kutangatanga,
 Bwana,
 Sasa naja nyumbani;
 Nitauamini upendo Wako, nitaliamini Neno
 Lako,
 Sasa naja nyumbani.

Naja nyumbani, naja nyumbani,
 Kamwe sitazurura tena;
 Ifungue kabisa mikono Yako ya upendo,
 Sasa, Bwana, naja nyumbani.

²¹² Na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi, kwa ajili ya jamaa hawa wadogo.

²¹³ Baba wa Mbinguni, kama kukiwapo na kesho inayokuja, kama Yesu atakawia kwa miaka mingine kumi ama kumi na mitano, hawa watakuwa ndio wavulana na wasichana ambao wataupeleka huu Ujumbe kwa vizazi vingine vijavyo. Sina shaka moyoni mwangu, Bwana, ila kwamba siku zote za maisha yao watakumbuka wakija kwenye haya madhabahu. Nao ni maskini vito vidogo, Bwana. Mioyo yao michanga na ya kitoto imehukumiwa asubuhi ya leo. Hata hawajausikia Ujumbe wote; ndio tu watoke mle chumbani, wakitoka kumsikia Dada yetu Arnold akinena; wakaja kuyazunguka madhabahu hapa, wakiyatao maisha yao madogo Kwako.

²¹⁴ Sasa, Baba, ndiyo kwanza nimalize kuzungumza ya kwamba ndani yetu mnakaa Roho Mtakatifu. Naye huyu Roho Mtakatifu, imani pamoja na huyu Roho, inafanya mambo yote. Nami ninaamini ya kwamba saa hii hasa, unasamehe kila dhambi waliyotenda. Nami ninakuomba Wewe, kwa imani yote iliyo moyoni mwangu, ya kwamba utayadumisha maskini maisha yao kote safarini. Jalia kamwe wasitangatange kutoka kwa Njia hiyo.

²¹⁵ Hili hakika ni jambo lisilo la kawaida. Roho alisema asubuhi ya leo, “tungeona jambo lisilo la kawaida.” Mungu, kama umeacha kuwashughulikia hao wengine, wachukue watoto wadogo. Jinsi ambavyo asubuhi ya leo, kwenye wito wa madhabahuni, hakuna hata mtu mzima mmoja, bali kundi zima la watoto wadogo limekuja huku. Hata hivyo, ulikuwa ni Ujumbe mkuu ulio mgumu kueleweka, hata kwa watu wazima, bali watoto hawa walishika Roho Yake. Tunakushukuru kwa ajili yao, Baba. Ninawakabidhi Kwako, kama mtumishi Wako, kama tunu za mkutano huu; kwa, tukikumbuka ya kwamba Uwepo udumuo wa Maji ya Uzima utabubujika pamoja nao mradi wangali hai. Jalia wapate imani sasa katika yale yanayotendeka,

kwamba Mungu aliyewavuta kutoka kitini na kuwatuma huku juu, jalia wawe na imani katika huyo Mungu siku zote za maisha yao. Jalia maskini roho zao ziletwe Kwako katika siku ya kufa kwao; zirudishwe kwenye mwili wao kwenye siku ya ufufuo. Hao ni Wako, Baba. Tunawakabidhi Kwako kupitia Jina la Yesu.

216 Huku tumeinamisha vichwa vyetu. Nitawauliza watoto hawa wote madhabahuni, wanaoamini ya kwamba Yesu ni Mwokozi wako na Ndiye aliyekwambia, huko nyuma katika wasikilizaji, uje hapa na kupiga magoti kuyazunguka haya madhabahu. Je! mnaamini ya kwamba Yesu anawapenda na ameisamehe dhambi yenu? Ninawatakeni ninyi nyote msimame kwa miguu yenu na mwangalie hapa nyuma kwenye wasikilizaji. Hii, hivyo ndivyo unavyoweza kuwaambia watu ya kwamba unaamini ya kwamba Yesu anakuokoa. Sasa simameni kwa miguu yenu, hiyo ni sawa, na mwangalie moja kwa moja huko nyuma kwenye wasikilizaji. Ninyi nyote wavulana wadogo na wasichana mnaompenda Yesu, simameni na muwageukie kusanyiko pale, kila mmoja wenu.

217 Vipi kuhusu ninyi wasichana wadogo hapa mbele? Mnaamini? Mnampenda Yesu? Hawa wasichana wadogo hapa, je! mnampenda Yesu kwa moyo wenu wote? Mnampenda? Mnampenda? Unampenda, kipenzi? Simameni hapa, acheni watu wajue ya kwamba mnampenda Yesu. Mungu awabariki.

218 Sasa hebu tugeuke upande *huu* na tuwaimbie watu hawa kabla hatujaondoka, “Yesu anipenda! Hili najua. Biblia inaniambia hivyo.” Mnaona? Hebu tuinue tu mikono yetu tunapouimba sasa. Vema, hebu tuuimbe.

Yesu anipenda! Hili najua,
Kwa kuwa Biblia huniambia hivyo;
Watoto wadogo ni Wake,
Wao ni wanyonge. . .

219 Sasa huku mmeinua mikono yenu, ni wangapi humu ndani wanataka—wanataka kuwapo?

Naam, Yesu anipenda,
Naam, Yesu anipenda,
Naam, Yesu anipenda,
Biblia inaniambia hivyo.

220 Sasa ninyi nyote fuatisheni nyuma yangu. Ninaamini [Watoto madhabahuni wanasema, “Ninaamini”—Mh.] Yesu Kristo [“Yesu Kristo”] ni Mwana wa Mungu. [“ni Mwana wa Mungu.”] Leo hii [“Leo hii”] ninamkubali kama mwokozi wangu binafsi. [“ninamkubali kama mwokozi wangu binafsi.”] Tangu leo, [“Tangu leo,”] na kuendelea, [“na kuendelea,”] nitampenda [“nitampenda”] na kumtumikia. [“na kumtumikia.”] Amina. [“Amina.”]

221 [Ndugu mmoja katika kusanyiko anasema, “Ndugu Branham, nina watoto wanne moyoni mwangu wakati huu.

Waweza kuwaombea tafadhali?”—Mh.] Hakika nitawaombea, Ndugu Ben.

²²² Baba wa Mbinguni, mtu huyu anawaona hao watoto wengine wadogo wakimjia Kristo, naye analia, kama baba, kwa ajili ya watoto wake wadogo. Naye Roho aliyewaleta hawa watoto wadogo madhabahuni, jalia Roho yuyo huyo awaokoe watoto wake, Bwana. Tujalie. Tunawakabidhi Kwako, Baba, katika Jina la Yesu Kristo.

²²³ Sasa wakati ninyi watoto wadogo mnaporudi kitini mwenu, ninataka kila mtu kwenye ile safu apeane mikono na hawa watoto wadogo, ama kuwapongeza wanaporudi. Nyote rudini vitini mwenu, upande *huu*. Na hebu kila mtu pale awapongeze jamaa hao wadogo. Nasi tunawapenda kwa mioyo yetu yote. Ninyi ni washiriki wa Mwili wa Kristo, mko tu ndani Yake kama wengine wetu.

Twenenda Zayuni,
Zayuni nzuri, nzuri;
Twenenda juu Zayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.

Njoni, sisi tumpendao Bwana,
Na acheni furaha zetu zijulikane,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Na hivyo mkizunguke kiti cha enzi,
Na hivyo mkizunguke . . .

Huo ni uimbaji mzuri sana! Hebu na tuinue mikono yetu sasa.

Twenenda Zayuni,
Zayuni nzuri, nzuri;
Twenenda juu Zayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.

Hebu na tupeane mikono sisi kwa sisi tunapimba sasa.

Twenenda Zayuni,
Zayuni nzuri, nzuri;
Twenenda juu Zayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.

²²⁴ Sasa hebu tusimame huku tumeviinamisha vichwa vyetu, wakati . . . Ucheze Ndugu Teddy, ninii tu . . . [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, *Twenenda Zayuni*—Mh.]

²²⁵ Nina haja kadhaa hapa, na leso na kadhalika. Huenda zimetoka kwenye nchi za ng'ambo. Billy alikuwa akiniambia walikuwa na jozi ndogo ya vijibuti kutoka kwa maskini mtoto mchanga huko Uingereza, urefu kama *huu*, maskini kijitoto hicho kimelemaa kabisa. Na kwa hiyo tulikuwa tumwombee huyo, pia.

²²⁶ Na kwa hiyo...[Katika kusanyiko, Ndugu Ben anasema, “Ndugu Branham, samahani kwa kuingilia, bali omba ya kwamba, yule aliyeligonga gari letu jana usiku, kwenye bamba langu la mkono wa kulia, omba ya kwamba hiyo itafunuliwa. Omba ya kwamba Bwana alifunue.”—Mh.] Amina, Ndugu Ben, hakika nitafanya hivyo.

²²⁷ [Ndugu Branham anaendelea kuuvumisha, *Twenenda Zayuni*—Mh.]

²²⁸ Tunapotembea kwa utaratibu, Bwana, tunajua ya kwamba Mwamba uliopigwa uko moja kwa moja pamoja nasi, Uwepo udumuo wa Maji yatokayo Mwambani unaambatana na Kanisa. Ee Mungu wa Milele, tufungulie, asubuhi ya leo, imani katika Mungu huyu aliye pamoja nasi. Ninajua utatufungulia, kadiri tu tunavyoweza kupata fadhili Kwako, kwamba unaweza kutuamini na Hiyo. Kama ukitupa Hiyo kwa wingi, huenda tukaitumia vibaya, Bwana. Bali tukipata neema Kwako, jalia itendeke.

²²⁹ Ndugu yetu alisema ya kwamba mtu fulani aliligonga gari lake. Ee Mungu, tunajua mtu huyu hana pesa kufanya mambo haya. Ninaomba ya kwamba utamfanya mtu huyo ajihisi ana hatia, ama chochote kile, aweze kutubu kwa kufanya jambo hili, aje, aseme, “Ndugu, nitalitengeneza gari lako, nililigonga.” Msaidie Ndugu Ben na wapendwa wake.

²³⁰ Hizi hapa zilizowekwa mkononi mwangu ni lesa na haja, tuna imani katika huyo Mungu. Musa alikuwa na imani katika Mungu huyo, naye akaivuka bahari. Danieli alikuwa na imani katika huyo Mungu, naye akatolewa kwenye tundu la simba. Shadraki, Mishaeli, na Abedinego, walikuwa na imani katika Yeye, nao wakauzima moto. Paulo alikuwa na imani katika Yeye, ndipo siku moja wakati ibada zilipokuwa ngumu sana naye Paulo asingeweza kumfikia kila mtu, yeye alichukua tu lesa, akasema, “Ninaamini ya kwamba Mungu yu pamoja nami.” Akaiweka mikono yake juu ya lesa hizo na nguo, nao pepo wachafu wakawatoka watu hao, na maradhi na magonjwa yakawaacha. Na, Mungu, nina imani katika Mungu yuyo huyo. Jalia pepo mchafu aondoke. Maradhi, magonjwa, mateso, jalia yaondoke, Bwana.

²³¹ Wewe Ndiwe Mungu yeye yule aliyenena nami huko chini kwenye ile Nguzo ya Moto, huko chini mtoni. Wewe Ndiye ambaye picha Yako uliyopigwa pamoja nami imetundikwa hapa, ukutani. Uko pamoja nasi, Bwana. Wewe upo daima, Nguzo ile ile ya Moto. Nasi tumeyafurahia Maji yatokayo Mwambani kila siku, tunapoungana katika Roho. Basi, Wewe upo hapa. Tuna imani Nawe, Bwana. Tuna imani Kwako. Tunaamini ya kwamba utatutia mafuta na kutusaidia. Si kwa ajili ya utukufu wetu, Bwana; tungekuwa kama Musa basi, wakati alipofanya jambo baya. Tunataka kufanya jambo la kukusaidia Wewe,

Bwana. Hilo ndilo kusudi la moyo wetu, kukusaidia Wewe, kama tunaweza kufanya hivyo. Wewe tuonyeshe, Baba, lolote unalotutaka tufanye.

²³² Na sasa, juu ya tendo la imani, ninayahukumu maradhi ambayo lesa hizi zinayawakilisha, na haja hizi. Yatawaondokea watu hawa. Ninajua utafanya hivyo, Bwana. Ninaamini hilo, moyoni mwangu, ya kwamba utalitimiza. Yaponye maradhi yote miongoni mwetu asubuhi ya leo.

²³³ Waokoe hao walioinua mikono yao, waliosema wangependa kuja kwenye Mwamba, wapate Maji. Mungu, hebu waone kiu sana leo, jalia kuwe na maisha yaliyokolea chumvi kwao, mpaka itawafanya kumwonea Kristo kiu. Tujalie.

²³⁴ Kuwa pamoja nasi usiku wa leo, Baba. Ee Mungu, jalia nitafute kujua, kupitia haja hizi, kile kilicho moyoni mwa watu hawa. Kama hamna kitu moyoni mwao, basi, Bwana, naomba unipe kitu cha kuihubiria mioyo yao usiku wa leo.

²³⁵ Mbariki Ndugu yetu Neville, pamoja na mke wake, familia yake; kanisa letu dogo, wadhamini wetu, mashemasi wetu, washiriki wetu. Na Mwili Wako kila mahali, kuwa pamoja nasi, Baba. Tunakabidhi hili mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo.

Zayuni; twenenda juu Zayuni,
Mji ule mzuri wa Mungu.

Sasa hebu na tuuimbe tu, vizuri, vizuri sana Kwake sasa. Mnaona?

Njoni, sisi tumpendao Bwana,
Na acheni furaha zetu zijulikane,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Na hivyo mkizunguke kiti cha enzi,
Na hivyo mkizunguke kiti cha enzi.

Pamoja na mioyo yetu iliyoinamishwa sasa.

Twenenda Zayuni,
Zayuni nzuri, nzuri;
Twenenda juu Zayuni,
Mji ule mzuri wa Mungu.



MAJI YALIYOPO DAIMA YATOKAYO MWAMBANI SWA61-0723M

(The Ever-Present Water From The Rock)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 23 Julai, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org